SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 3

**WAFANYABIASHARA** walalamikia EFD kukwama kutoa risiti




UKURASA 11

Nipashe

Jumatatu Novemba 29, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580779

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Samia: Uhusiano wa kidiplomasia umeimarika

**VIKWAZO** kibiashara Kenya, Uganda, Tanzania vimeondolewa...*Endelea ukurasa wa 2*



## Waziri: Ukame umeua mifugo na wanyama

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, baada ya kufunga kongamano la wafanyabiashara wa Tanzania na Uganda lililofanyika katika viwanja vya Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# TMA yazungumzia neema ya mvua

UKURASA 2

MICHEZO KOCHA KMC SASA KUFUNGIA KAZI BEKI UK.20 MAONI, KATUNI UK.6

# TMA yazungumzia neema ya mvua

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema kuwa mvua zilizoanza kunyesha nchini ni endelevu, huku wananchi wakitakiwa kufuatilia taarifa za utabiri unaotolewa.

Hali hiyo inakuja baada ya TMA kutoa utabiri Oktoba mwaka huu, kueleza kuwa jua la utosi limeingia nchini, hali iliyosababisha kuongezeka kwa joto, huku mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Ruvuma ikirekodi kiwango cha juu cha joto na kuongezeka kwa ukame uliosababisha mifugo na wanyama kufa.

Katika utabiri huo TMA ilisema kuwa kutakuwa na kipindi cha ukame huku mvua zikitarajiwa kuanza kunyesha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi huu.

Kwa sasa mvua zinanyesha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro, Mwanza na Rukwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Kituo Kikuu cha Utabiri cha TMA, Samuel Mbuya, alisema mvua zilizoanza kunyesha zilizotabiriwa kwenye utabiri wa TMA wa Oktoba mwaka huu.

"Hizi ni mvua zile ambazo tulizitabiri, na zimeanza sasa kunyesha, kikubwa tunawaomba wananchi na wadau wote kufuatilia utabiri wetu wa kila saa na kila siku ambao tunautoa kila siku," alisema Mbuya.

Aidha, alisema mvua hizo zinatarajia kuendelea kama ambavyo walitabiri.

"Bado hakuna mabadiliko makubwa, tunatarajia mvua zitaendelea kusambaa kwenye maeneo mbalimbali, TMA tutaendelea kutoa taarifa ili wananchi wafahamu na kuchukua tahadhari," alisema Mbuya.

Kutokana na kuongezeka kwa ukame viongozi mbalimbali wa dini wamefanya ibada ya kuomba mvua, huku Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), likitangaza kupungua kwa uzalishaji wa umeme kwa megawati 345 sawa na asilimia 21 kwenye vituo vyake vitatu vya Kihansi, Kidatu na Pangani.

Aidha, katika baadhi ya maeneo kuna mgawo wa umeme, huku wengine wakilazimika kutumia majenereta kupata nishati, na TANESCO ilieleza kuwa inaelekeza nguvu kwenye umeme wa gesi ili kuzalisha megawati 358.

Pia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), ilitangaza ratiba ya mgawo wa maji maeneo mbalimbali kutokana na kupungua kiasi cha maji Mto Ruvu, huku Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiagiza kuchukuliwa maji ya bwawa la asili ili kuongeza kiasi cha maji kwenye mto huo.

Hatua nyingine ni kupiga marufuku shughuli za kilimo na kupepusha maji Mto Ruvu.

Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni aliziagiza kamati za ulinzi na usalama kusimamia na kulinda vyanzo vya maji dhidi ya uharibifu, ambao umechangia ukame.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akizungumza na Uongozi wa Jumuiya ya UMAWA Zanzibar, katika ukumbi wa Ikulu jijini Zanzibar na (wapili kulia) Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Mussa Miraji Vuai, akiwa na ujumbe wake. **PICHA: IKULU**

# Samia: Uhusiano wa kidiplomasia umeimarika

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania, Uganda na Kenya umeimarika kwa kuondoa vikwazo vya kibiashara vilivyochangia kuzorota kwa biashara.

Akizungumza jana kwenye kongamano la biashara kati ya wafanyabiashara wa Uganda na Tanzania lililofanyika jijini Dar es Salaam, alisema mvutano wa kibiashara baina ya nchi hizo ulikuwa unafukuta kwenye mipaka na kuathiri shughuli nyingi za kiuchumi.

"Wafanyabiashara wa Tanzania ni mashahidi, tulikuwa tunavutana hapa na Kenya, kila kinachokwenda hakipiti, kule hakipiti na huku hakipiti," alisema Rais Samia na kuongeza;

"Kule wakizuia na Mkuu wa Mkoa huku kwetu na yeye anasema kuanzia leo na sisi hakipiti. Lakini tulikaa tukaelezana ukweli, tulikuwa tunachomeana kuku mipakani, dhambi tupu viumbe wa Mungu, mnamwaga petroli mnachoma, haikuwa na maana. Tumeondosha vikwazo na sasa biashara imekua mno, ukiangalia 'figure' (takwimu) za biashara, Kenya na Tanzania imekua mno."

Aidha, alisema kama ambavyo biashara imekua kwa upande wa Kenya na Tanzania, ni muhimu ikakua kati ya Uganda na Tanzania.

Kwa mujibu wa Rais Samia, Tanzania iko tayari kununua sukari Uganda kama nchi hiyo ilivyoomba.

"Tunataka biashara ikakue kwa upande wa Uganda pia, ikakue kwa upande ule, mheshimiwa Rais Museveni, amesema hapa kwamba aliomba sisi tununue sukari kwake, lakini walisikia 'statement' (taarifa) za waziri wetu kuwa hatutanunua, hatutakubali... tutanunua sukari kutoka Uganda," alisema Rais Samia.

Alisema pamoja na nchi hizo za Tanzania na Uganda kujitahidi kwenye eneo la uwekezaji, lakini bado hazifanyi vizuri na kwamba nguvu kubwa inahitajika kuongeza jitihada zaidi.

"Lakini tunapozungumzia uwekezaji ni lazima uendane na maendeleo endelevu ya kiuchumi na mifumo inayoimarishwa katika kujenga uwezo wa uzalishaji wa ndani wenye kuunganisha juhudi za kila sekta ya uchumi. Kumudu kwa kiwango kikubwa cha mahitaji ya soko la ndani na ushindani wa bidhaa kutoka nje," alisema Rais Samia.

"Nchi zetu zimejaliwa kuwa na rasilimali au maliasili nyingi ambazo hazijatumika ipasavyo kwa madhumuni ya kukuza uwekezaji, hivyo ni muhimu kuendelea kuvutia uwekezaji katika nyanja mbalimbali, ikiwamo viwanda vinavyotumia malighafi za ndani hususani kwenye sekta za kilimo na maliasili, viwanda vinavyozingatia fursa za kijiografia, vinavyotumia nguvu kazi zaidi ili kuzalisha ajira."

"Vinavyoendana na ukuaji wa miji, vinavyozalisha bidhaa kukidhi mazingira ya biashara na kuwekeza zaidi kwenye rasilimali watu pamoja na vinavyozalisha viwanda vingine ikiwamo viwanda vya mbolea na kemikali vinavyotokana na by product za mafuta na gesi."

Kwa mujibu wa Rais Samia, serikali inaendelea kufanya maboresho muhimu ya kimuundo na kisheria ili kuhakikisha kunakuwa na urahisi wa kuanzisha na kufanya biashara na uwekezaji.

Rais Samia alisema watahakikisha wanamaliza vikwazo au kuondoa kabisa vikwazo vyote visivyo vya kikodi, kuhakikisha usalama wa mitaji na uhakika wa kutengeneza faida kwa wawekezaji wanaowekeza Tanzania.

Aidha, alisema hivi karibuni Tanzania itafungua ofisi ndogo ya Mamlaka ya Usimamizi Bandari Tanzania (TPA) Kampala, Uganda ili kusogeza huduma karibu.

Pia, aliwahamasisha wawekezaji waende kuwekeza Uganda na wa nchi hiyo kuja kuwekeza nchini.

Rais Samia aliwataka wafanyabiashara wa nchi hizo mbili kumaliza tofauti zilizokuwapo miaka ya nyuma ili kukuza ushirikiano utakaoimarisha biashara kwa manufaa yao binafsi na nchi zao.

"Kule nyuma mlikuwa mnavutana watu wa serikali ya huku, na serikali ya kule, wafanyabiashara na wa huku na wa kule, badala ya kukaa na kuangalia vikwazo ni vipi na vipi tutaondosha, mlikuwa mnavutana na kuwekeana kauzibe, asije na nyie msiende, hiyo haisaidii upande wa Uganda wala Tanzania," alisema na kuongeza;

"La maana ni kuondosha vikwazo na kusonga mbele, kwa hiyo niwaombe muwe mnakutana mara nyingi ili kujadli namna ya kumaliza tofauti zenu na kuendeleza zaidi biashara zenu."

"Tumewataka mawaziri wakutane haraka kwenye ile tume yetu ya pamoja ya ushirikiano waangalie changamoto tulizozizungumza ili ziondoshwe, ili nanyi wafanyabiashara mkijua kwamba serikali imeondosha vikwazo, nanyi mwondoshe vya kwenu ili mfanye kazi kwa haraka na tuone matokeo ya haraka."

Kwa upande wake, Rais Yoweri Museveni, aliiomba sekta binafsi za nchi hizo kushirikiana na serikali zao katika kuwekeza na kuendeleza biashara katika nchi zao.

"Sekta binafsi ndiyo tegemeo kubwa katika nchi yoyote katika kujenga na kuimarisha uchumi, kwa hiyo ushirikiano wake unahitajika zaidi katika kuhakikisha jambo hili linafanikiwa," alisema Museveni.

Alisema kuna haja ya kutumia rasilimali zilizopo katika nchi hizo mbili kukuza uchumi wake na kwamba pamoja na kujaliwa kuwa nazo bado hazitumiki ipasavyo.

## Watoto watatu wa familia moja wafa madai kula kasa

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

WATOTO watatu wa familia moja wamefariki dunia baada ya kula samaki aina ya kasa anayedhaniwa kuwa na sumu, huku watu 22 wakiwa wamelazwa katika Hospitali ya Kotege wilayani Micheweni Mkoa Kaskazini Pemba.

Kamanda wa Polisi Mkoa Kaskazini Pemba, Kamishna Msadizi Juma Said, alisema tukio hilo la familia zipatazo 10 kula samaki huyo lilitokea Taponi Msuka katika Wilaya Michweni.

Aliwataja watoto waliokufa ni Asma Seif Mzee (4), Firdaus Seif Mzee (4) na Sabiha Ali Shaal (4), wote wakazi wa Taponi Msuka, ambao baba yao ni dalali wa samaki katika Bandari ya Msuka.

Kamanda alisema watoto wawili Mzee Seif Mzee na Farhati Shaibu Mzee waliolazwa hospitalini hali zao ni mbaya kati ya familia 10 za Taponi waliokula samaki huyo.

Kamanda Said alisema kati ya watu 22 waliolazwa, watano wana umri kati ya miaka 30 hadi 70 na 17 ni kati ya miaka miwili hadi 29, huku wengi walioathirika ni watoto wadogo.

Ilielezwa kuwa wengi baada ya kula samaki hiyo waliendelea kuugua bila kwenda hospitali.

Mbunge mstafu wa Jimbo la Chambani, Yusufu Salimu Husein, aliyekuwapo katika eneo la tukio aliwapongeza madaktari kufika na kutoa msaada kwa waathirika.

Alisema kuja kwa wingi kwa madaktari ni jambo jema linalotia matumaini ya kupata huduma stahiki wagonjwa hao, ila alisema inatia shaka kuwapo kwa vifaa na dawa za kutosha kutokana na tukio kutokea ghafla.

Matukio ya watu kula samaki aina ya kasa na kufariki dunia kisiwani Pemba hutokea mara kwa mara. Miaka michache iliyopita huko Vitongoji katika Wilaya ya Chakechake na Kiuyu Mbuyuni watu kadhaa walikufa baada ya kula kasa.

# Waziri: Ukame umeua mifugo na wanyama

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema nchi inakabiliwa na ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, na kwamba baadhi ya matatizo yameanza kujitokeza ikiwamo vifo vya wanyama.

Athari nyingine ni baadhi ya visiwa kuwa hatarini kupotea na mikoa mitatu mikubwa imekumbwa na mgawo wa maji.

Jafo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kushiriki mbio za baiskeli za kilometa 10 zilizoandaliwa na Umoja wa Ulaya (EU) nchini kwa kushirikiana na Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam (UWABA).

Mbio hizo ambazo zilihusisha makundi tofauti ya watoto, wanawake, wenye ulemavu, watu wazima na viongozi zimelenga kuunga mkono serikali katika kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Waziri Jafo alisema hali ya ukame inashamiri kila mahali na wameendelea kupata taarifa kwenye baadhi ya mikoa, ng'ombe na mbuzi wanaendelea kufa.

"Leo hii Jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro yamekumbwa na mgawo mkubwa wa maji kwa sababu maji yamezidi kupungua," alisema.

Waziri huyo alisema ni lazima mazingira yatunzwe kwa sababu wakiangalia kiwango cha maji, bahari inazidi kupanda na huko visiwani Pemba hali inazidi kuwa mbaya.

"Baadhi ya visiwa vipo hatarini kutoweka hii yote ni suala la mabadiliko ya tabianchi. Ujumbe wetu, tuendelee kutunza mazingira ili tuendelee kupata maji.

"Jana (juzi), tulikuwa katika mdahalo mkubwa kuhusu suala la mazingira na mabadiliko ya tabianchi, takwimu za maji zinavyosema, kiwango cha maji kinachoingia Jiji la Dar es Salaam kimepungua kwa kiwango cha nusu ikilinganishwa na hali ya kawaida, yote haya ni kutokana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Jafo aliendelea kuzisisitizia halmashauri kila moja inatakiwa kupanda miti milioni 1.5 lengo ni kwa mwaka kuwe na miti milioni 276 sawasawa katika halmashauri 184.

Katika mbio hizo waziri huyo alisema amebaini baadhi ya miundombinu ya barabara mvua ikinyesha maji hayapiti kwenye mitaro na kusababisha kujaa barabarani.

"Naomba nilichukue hili nitawasiliana na TARURA (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) na TANROADS (Wakala Barabara Tanzania) nimeona eneo la barabara ya Muhimbili lina tatizo kubwa la maji ikiwezekana mifereji yake ifunuliwe maji yapite," alisema.

Aidha, alimpongeza Balozi wa EU, nchini, Manfredo Fanti, kwa uratibu wa mbio hizo ambazo zinahamasisha wananchi suala la utunzaji wa mazingira, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri binadamu, wanyama na mimea.

Balozi wa EU, nchini, Fanti alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakishirikiana na serikali katika eneo la utunzaji mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Ujumbe wetu kwa jamii watambue baiskeli ni usafiri mzuri na watu wanautumia kila siku, lakini wakati mwingine watumiaji wanakutana na matatizo barabarani kupitia vyombo vya moto, ujumbe wetu watambue baiskeli inatunza mazingira mijini," alisema.

Balozi Fanti alisema kampeni ya kustahimili mabadiliko ya tabianchi waliianza mwezi Mei kwa maonyesho yaliyofanyika Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam.




Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, akiwasilisha taarifa ya mafanikio na mwelekeo wa sekta ya kilimo kwa waandishi wa habari jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# W/biashara walalamikia EFD kukwama kutoa risiti

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wamesema wamekuwa wakiingia katika migogoro na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa wa kikodi Kahama, kutokana na kutotoa risiti ya bidhaa wanazouza kwa wateja wao kutokana na mashine za kieletroniki wanazotumia kujaa na kushindwa kutoa risiti.

Malalamiko hayo waliyabainisha jana wakati wa semina ya wafanyabiashara kwenye mabadiliko ya sheria na uwasilishaji wa ritani kwa njia ya kielektroniki kwa kushirikisha wafanyabiashara 152 kutoka halmashauri za Msalala, Ushetu na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Nirraj Kakad, alisema amekuwa akipata matatizo ya kutumia mashine hiyo kwani wakati mwingine inagoma kutoa risiti baada ya kuonekana imejaa na kusababisha kuwapatia wateja wake risiti ya mkononi, hali ambayo ni kinyume cha sheria.

Aliiomba TRA mkoa wa kikodi Kahama kumweleza ni njia gani ya kufanya ili kuondokana na tatizo hilo ambalo mwisho wa siku linaweza kumwingiza matatani na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa kutokutumia mashine hiyo vyema.

Akijibu malalamiko hayo Ofisa Mwandamizi wa TRA, Allex Mambenja, alisema wameandaa mfumo mpya wa kielektroniki ambao utakuwa haujai na utawasaidia katika utoaji wa risiti na uandaaji wa ritani kwa kutumia simu za mkononi (janja).

Aidha alisema, kwa wafanyabiashara ambao mashine za kielektroniki ambazo hazijawaleta matatizo yoyote waendelee kuzitumia pamoja na kuwapo kwa mfumo huo mpya kwani hauathiri chochote katika biashara zao na kwa wale ambao hawatumii vema mashine watachukuliwa hatua za kisheria.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara na Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Shinyanga, Dk. Meshaki Kurwa, alisema Mji wa Kahama umekuwa ukikua kwa kasi, hali ambayo wafanyabiashara wanatakiwa kutengenezewa miundombinu rafiki ya kufanya biashara zao ili kupata faida na kukuza mitaji yao.

Pia alisema, wamekuwa wakichukua wafanyabiashara kutoka mikoa mbalimbali na kuwapeleka nchi za nje zilizoendelea kibiashara kwenda kujifunza namna bora ya kuwa na bidhaa zenye ubora na zinazokidhi hali ya masoko ya kimataifa.

Katibu Tawala wa Wilaya, Timoth Ndanya ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye semina hiyo, aliishukuru TRA kwa kuiletea sifa wilaya hiyo kwa kufanya vema kwenye ukusanyaji wa kodi na kuwa washindi wa kwanza kitaifa kwa mwaka jana.


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**
**Kituo Cha Mjini Mkoa wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na 323/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU ABDALLAH MUSSA MKAMBARA WA MOROGORO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RAJABU ABDALLAH MKAMBARA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 08 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

**Zingatia**

Endapo Kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa Leo 08 Mwezi 11 Mwaka 2021

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116591802



**KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI**

**WANSANGLA WILLIAM MICHAEL**
Anatangaza kupotea kwa Kadi ya **PIKIPIKI (trycle) MC 122** na Kadi za Magari ya Chuo Cha JORDAN, Toyata **LAND CRUISER** Plate **NO T491ATC,** Toyota RAV4 PLATE NO 713BZR, Toyota RAV4 PLATE NO **791 BZC,** TRACTOR **T797,** TRAILLOR **T 322** AFY, Toyota COASTER **T790 BZC ,** NISSAN DATSUN **T331 AFY.** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa Kituo chochote Cha polisi RB Namba.
**MOR/MOR/RB/527902/2021**

116591402

HABARI KITAIFA

# Mbaroni tuhuma kukutwa na nyara

**Na Neema Hussein,** KATAVI

JESHI la Polisi mkoani Katavi linamshikilia Seda Mbutula (47) kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali.

Nyara hizo za serikali ni mafuta ya simba, magambaya kakakuona, ngozi ya paka pori, vipande vinne vya meno ya ngiri na mkia mmoja wa nyumbu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Katavi, Ali Hamad alisema, tukio hilo limetokea Novemba 23, mwaka huu katika Pori la Akiba Rungwa lililoko Kata ya Ilunde Wilaya ya Mlele.

Hamad alisema baada ya operesheni maalumu walifanikiwa kumkamata mtu huyo akiwa amehifadhi nyara hizo kwenye mfuko wa salfeti na kuficha ndani ya nyumba yake.

Alisema pia Jeshi la Polisi limemkamata Samuel Kazambi (36) kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya yadhaniwayo kuwa ni bangi.

Kamanda Hamad alisema tukio hilo lilitokea Novemba 24, mwaka huu, katika kijiji cha Milala Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi akiwa na bangi jumla ya kete 12 na mbegu za bangi zenye uzito wa gramu 1,000 ambazo alihifadhi ndani ya nyumba yake. Alisema operesheni hiyo ilianza Novemba 11 na inatarajiwa kumalizika Novemba kesho na kwamba wote watakaozisalimisha silaha zao ndani ya muda huo watapewa msamaha wa kutokushtakiwa.

Hamad alisema upelelezi unaendelea na utakapokamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Said (watatu kulia), akifafanua jambo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini, Wakili Julius Kalolo (wapili kushoto), Mjumbe wa Bodi, Oswald Urassa (kushoto) na wataalamu kutoka REA na TANESCO, wakati ujumbe huo ulipokuwa katika ziara ya kikazi wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, mwishoni mwa wiki. **PICHA: VERONICA SIMBA**

# Benki kuongeza ukopeshaji sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya ukopeshaji nchini kuathirika kutokana na janga la Uviko-19, benki zimeahidi kuongeza mikopo kwa ajili ya sekta binafsi.

Hatua hiyo imeelezwa imetokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia na hatua zinazochukuliwa na serikali kuweka sawa huduma hiyo.

Taasisi hizo za fedha ziliweka bayana mpango huo mwishoni wa wiki jijini Dodoma kwenye Mkutano wa 20 wa Taasisi za Fedha (COFI 2021) na kusema kuimarisha ukopeshaji kutasaidia uzalishaji na kuukwamua uchumi wa taifa kufuatia janga la Uviko-19.

Kwa mujibu wa viongozi waandamizi wa benki hizo, hilo litawezekana kwa sababu benki nchini zina uwezo kifedha kukopesha zaidi na tena kwa riba rafiki.

Ili yote hayo yaweze kufanyika kwa ufanisi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema juhudi za pamoja ni muhimu na ushirikiano wa wadau wote unahitajika.

"Janga la Uviko-19 limekuwa na athari kubwa kwenye benki zetu kuikopesha sekta binafsi," Zaipuna aliwaambia washiriki wa COFI 2021 wakati anawasilisha maada kuhusu kuongeza mikopo kwa sekta binafsi baada ya janga la Uviko-19.

Wasilisho lake lilijikita kwenye wajibu wa serikali, taasisi za fedha na sekta binafsi katika kuongeza upatikanaji wa mikopo na mchango wa wadau hao kufufua ukuaji wa uchumi.

"Ili kuchochea ukopeshwaji wa sekta binafsi baada ya janga la Uviko-19, mambo kadhaa yanabidi kufanywa na wadau husika. Hatua hizi zinahitaji mbinu shirikishi ili kuhakikisha matokeo endelevu ya kiuchumi," alisisitiza Zaipuna.

Aidha, alisema tayari kuna mazingira wezeshi ya kuongeza mikopo na ustahimilivu stahiki wa kisekta wa kuchochea kufufua ukopeshaji.

Hii ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia ambao baada ya kupigika na uviko hadi kudorora kwa asilimia 3.1 mwaka 2020 sasa Shirika la Fedha Dunia (IMF) linasema utakua kwa asilimia 5.9 mwaka huu. Kuimarika huko kutapelekea uchumi wa Tanzania nao pia kufanya vizuri ukikua kwa asilimia tano mwaka huu ukilinganisha na ukuaji wa 2020 wa asilimia 4.8.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, alisema hali itakuwa nzuri zaidi 2022 kutokana na kupungua kwa athari za Uviko-19 kutakopelekea uchumi wa taifa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka kesho. Mkutano wa 20 wa Taasisi za Fedha uliofunguliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan uliandaliwa na BoT kwa kushirikiana na Umoja wa Benki nchini (TBA) ili kujadili uimarishaji wa uchumi wa Tanzania kufuatia janga la Uviko-19.

Zaipuna alisema sababu nyingine ya kuwapo mazingira sahihi ya kufufua ukopeshaji ni kutokana na sera sahihi za serikali ambazo pamoja na kutoa kinga madhubuti dhidi ya Uviko-19 pia zimesaidia sekta ya benki kustahimili vishindo vya janga hilo.

Ustahimilivu huo ulipelekea raslimali fedha za benki nchini kuongezeka kwa asilimia 4.16 mwaka 2020 hadi Sh. trilioni 34.68 huku amana nazo zikiongezeka karibu kwa asilimia nne hadi Sh. trilioni 24.77.

"Hali hii ilizifanya benki kuendelea kulihudumia taifa kipindi chote za janga la Uviko-19 bila kuathiri wateja na wafanyakazi wake," Zaipuna alisema na kuongeza kuwa taasisi hizo pia zilichangia juhudi za taifa za kukabiliana na Uviko kwa kuchangia zaidi ya Sh. bilioni moja. Benki zilihimiza matumizi mbadala ya kufanya malipo na kupanua wigo wa huduma za kifedha za kidigitali kwa kuongeza vikomo vya miamala na kufuta kabisa baadhi ya tozo.

# PM awapa ma-RC zigo vyumba vya madarasa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wakuu wa mikoa yote kuhakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na miundombinu mingine ya elimu ambayo Serikali Kuu imeipatia fedha inakamilika kabla ya Desemba 15, mwaka huu.

Alitoa agizo hilo jana wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya alipofanya ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kayuki na Chuo cha Uwalimu cha Msasani.

Waziri Mkuu aliwataka viongozi hao kila mmoja kusimamia miradi hiyo kwenye eneo lake la utawala ili wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari mwezi Januari wasikwame kwa sababu ya kutokamilika kwa vyumba vya madarasa.

Alisema serikali imeshatoa fedha nyingi za miradi hiyo zikiwamo za utekelezaji wa miradi ya Uviko-19 na kwamba lengo ni kuhakikisha matatizo ya sekta ya elimu yanapungua na wanafunzi wanasoma katika mazingira rafiki.

"Usipokamilisha miradi hiyo utakuwa umeshindwa kuleta matokeo chanya ambayo ndilo lengo la serikali, na usipoleta matokeo chanya tutakuwa wakali sana kwenye eneo hili, kwa hiyo nimeamua nitoe meseji kwenu leo," alisema Majaliwa.

Hata hivyo amewataka viongozi hao kuhakikisha miradi hiyo inajengwa kwa viwango vinavyoendana na kiwango cha fedha zilizotolewa na kwamba ili kufikia lengo hilo ni lazima wahakikishe vifaa vinavyotumika ni bora.

Baada ya kutembelea vyumba vya madarasa katika Shule ya Wasichana ya Kayuki pamoja na Chuo cha Uwalimu cha Msasani, Majaliwa aliwapongeza wasimamizi wa miradi hiyo kwa madai kuwa waliisimamia vizuri na imejengwa kwa viwango.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema walipokea zaidi ya Sh. bilioni 15.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, miundombinu ya barabara pamoja na miundombinu ya afya.

Vilevile alisema hivi karibuni walipokea Sh. bilioni 1.7 ambazo zinatokana na tozo za simu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika halmashauri mbalimbali za mkoa huo.

"Maagizo yako Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeyapokea na tutayatekeleza, lakini kwa zile fedha za tozo tumeshaanza kujenga vituo mbalimbali vya afya kikiwamo cha Kata ya Ndato," alisema Homera.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuboresha miundombinu ya elimu ikiwamo vyuo vya ualimu, shule za msingi na sekondari.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## OMBI LA KUONESHA NIA UTENGENEZAJI NA USAMBAZAJI WA MABATI
## KUMBUKUMBU: 0010007287

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya utengenezaji na usambazaji wa mabati katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Utengenezaji na Usambazaji wa Profaili za Mabati kulingana na viwango, vipimo na maelezo yaliyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na mkusanyiko wa mabati itazingatia EAS 468; 2019 Kiwango cha Afrika Mashariki cha mabati yaliyopakwa rangi ya awali - Maelezo, pamoja na marekebisho yake ya hivi punde, isipokuwa ikiwa imebainishwa vinginevyo.

**TAARIFA ZA JUMLA ZA BATI/PAA**

- Nguvu ya Mavuno ya Chuma: 550MPa
- Kiwango cha Mipako ya Aluminium-Zinki kwenye chuma: AZ85
- Uzito wa rangi: Mikroni 19
- Unene wa geji ya bati: 28G (0.32mm)
- Wasifu: Ubavu wa Kisanduku Uliogeuzwa
- Upana wa bati: 800mm - 1100 mm

**VIGEZO MUHIMU:**

- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha uundaji wa mabati katika kiwanda cha Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora kulingana na ISO 9001:2015.
- MSAMBAZAJI atatakiwa kuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha uzalishaji wa mabati cha uzalishaji cha mita za mraba 2100 za mabati kwa mwezi ili kukidhi kalenda ya matukio ya KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa wa kima cha chini cha jumla ya mita za mraba 17,000 za mabati, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha mita za mraba 2100 kwa mwezi.
- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha utengenezaji wa mabati ambazo zitakazoidhinishwa katika eneo la Mtengenezaji/kiwanda kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora sawasawa na viwango vilivyoainishwa.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji wa mabati hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Mabati pamoja na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 10 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au kimataifa
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:
- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

---

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **10 Disemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe ni **0010007287.**

---

**Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.**

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## OMBI LA KUONESHA NIA UTENEGENEZAJI NA USAMBAZAJI WA MILANGO
## KUMBUKUMBU: 0010007286

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya Utengenezaji na Ugavi wa Milango katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa minane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za Utengenezaji na Ugavi wa Milango kutoka kwa mbao aina ya 'Mpodo' au aina nyingine itakayoidhinishwa.

**VIWANGO:**

Nyenzo, uzalishaji na uunganisho wa muundo wa mbao utazingatia viwango vifuatavyo: BS 4978 – Uainisho wa Nguvu ya Kuonekana ya Mbao; BS 5268 - Matumizi ya Kimuundo ya Mbao; BS 6446 - Maelezo ya Utengenezaji na Ugandisho wa Mbao.

Masahihisho ya hivi punde kama yalivyorekebishwa mara kwa mara na Taasisi ya Viwango ya Uingereza yatatumika na MTENGENEZAJI atahakikisha kwamba masahihisho na marekebisho yote ya hivi punde zaidi yametolewa kwa KAMPUNI.

**VIPIMO:**

Mlango wa paneli nene wa 40mm ukubwa wa jumla wa 900 x 2100mm juu, unaojumuisha 120 x 40mm staili, reli za juu, za kati na za chini katika paneli mbili za chini na za juu na fremu ya mlango nene 100 x 45mm; pamoja na vifungio vyake husika kama yalivyotengenezwa na 'ASSA ABLOY' au kampuni nyingine yenye ubora unaofanana (bawaba za kitako cha shaba,pamoja na kitasa cha leva mbili).

Mlango wa paneli nene wa 40mm ukubwa wa jumla wa 800 x 2100mm juu, unaojumuisha 120 x 40mm staili, reli za juu, za kati na za chini katika paneli mbili za chini na za juu na fremu ya mlango nene 100 x 45mm; pamoja na vifungio vyake husika kama yalivyotengenezwa na 'ASSA ABLOY' au kampuni nyingine yenye ubora unaofanana (bawaba za kitako cha shaba,pamoja na kitasa cha leva mbili).

**VIGEZO MUHIMU:**

- MSAMBAZAJI atakuwa na uwezo wa kiwango cha chini cha uzalishaji cha milango 180 kwa mwezi ili kukidhi kiwango kitakachohitajika na KAMPUNI. KAMPUNI inategemea kuwa na uhitaji wa angalau milango 1500 kwa jumla, kwa kiwango kilichoainishwa hapo juu cha milango 180 kwa mwezi.
- KAMPUNI inahifadhi haki ya kuthibitisha utengenezaji wa milango itakonayo na mbao aina ya 'Mpodo' au aina nyingine ambazo zitakazoidhinishwa katika eneo la Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora sawasawa na viwango vilivyoainishwa.
- Hakuna nyenzo au viambatisho vitatumika katika utengenezaji hadi kibali cha awali cha matumizi yake kitolewe na KAMPUNI; wala mabadiliko yoyote katika asili, ubora, aina, na aina, chanzo cha usambazaji hakitafanywa bila ruhusa ya KAMPUNI.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejesho yajayo.
- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika.
- KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.
- Madirisha na maunzi yake yote yatakuja na dhamana ya vifaa na utengenezaji kwa muda wa miezi 12 tangu tarehe ya kukabidhi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au kimataifa
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:
- Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya ndani, 2017 na ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

**Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.**

---

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **08 Disemba 2021.** Kichwa cha barua pepe ni **0010007286.**

---

**Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, TPLB wamulike marefa hawa kulinda ubora Ligi Kuu

**HAKUNA** ubishi Ligi Kuu Bara imekuwa kivutio kikubwa kwa watazamaji katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati na nidhahiri kushika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika imestahili.

Kwa kulitambua hilo, tuna kila sababu ya kutoa kongole kwanza kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB), wadau wote wa soka hususan wadhamini kuanzia ngazi ya klabu hadi wa ligi hiyo pamoja na mashabiki wote kwa kuiunga mkono.

Wote tunatambua namna TFF na TPLB walivyotumia nguvu kubwa kuwashawishi wadhamini hadi kuandika historia kwa mara ya kwanza tangu ligi hiyo kuanzishwa nchini kuwapo kwa wadhamini wakubwa zaidi ya watatu walikubali kudhamini Ligi Kuu kwa mabilioni ya shilingi.

Lakini Watanzania kugeukia kuangalia mechi za Ligi Kuu Bara na kuacha ligi pendwa kama ya England, Hispania, Italia, Ujerumani na Ufaransa au wakati mwingine inapolazimu kuangalia zote kwa pamoja, hakika si kazi ya mchezo iliyofanywa katika kuiboresha na kuwa na mvuto.

Ubora huo pia umechangia kuzidi kuongezeka wachezaji wengi wa kigeni wanaovutiwa kuja kucheza soka nchini na si Ligi Kuu tu bali hata Ligi Daraja la Kwanza (Championship) kwa sasa wapo wageni wengi na wameongeza ushindani huko na viwango vya wachezaji wazawa.

Haya yote ni kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa katika klabu zetu hususan za Ligi Kuu, hivyo wachezaji na klabu za Championship kwa pamoja wanatamani kupanda kucheza Ligi Kuu ili kufaidi matunda hayo ya uwekezaji.

Tunaamini 'keki' iliyopo Ligi Kuu Bara ni tamu na ndiyo maana wachezaji mbalimbali wanavutiwa kuja kucheza hapa nchini, tena kutoka mataifa ambayo hapo mwanzo wakitoka kwao ni walikuwa wanakwenda moja kwa moja Ulaya ama nchi za Kiarubu kuliko na malipo mazuri.

Lakini kwa sasa Ligi Kuu kuna wachezaji kutoka Senegal, Mali na Ghana mataifa ni mara chache wachezaji wake kutoka kwao kucheza Afrika hususan ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Pia katika Klabu ya Simba kwa sasa tunashuhudia mchezaji ambaye ametoka kucheza michuano ya kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, Peter Banda, akiwa na FC Sheriff Tiraspol ya Moldova, ingawa tangu ajiunge na 'Wekundu wa Msimbazi' hao, bado hajapata nafasi ya kutosha kuonyesha uwezo wake, hayo yote ni matunda ya kuongezeka ubora wa Ligi Kuu.

Kutokana na ongezeko la nyota hao nchini, ni wazi ligi yetu itaendelea kutupiwa jicho kila kona barani Afrika na hata Ulaya kwa mawakala kuja kufuatilia vipaji ili kuvitafutia soko. Hivyo, huu ni wakati kwa TFF, TPLB kuongeza umakini na kuchukua hatua kali kwa wote ambao wanataka kuitia doa hususan waamuzi, ambao wakati huu ikiwa ndiyo ipo raundi ya saba msimu huu, malalamiko ya kutotenda haki yamekuwa mengi kwao.

Tunatambua yapo makosa ya kibinadamu na ndiyo maana hata wenzetu barani Ulaya, Asia na kwingineko, wamekuwa wakitumia teknolojia ya video ya kumsaidia refa (VAR) ili kuondoa utata ama lawama. Lakini pamoja na kutotumia VAR katika ligi yetu, yapo makosa mengi ya wazi ambayo yamekuwa yakifanywa na baadhi ya waamuzi kwa makusudi ama mapenzi yao kwa baadhi ya klabu au pengine huenda ni kwa maslahi yao binafsi, hivyo kwa marefa hawa, hawana budi kuchukuliwa hatua kali.

Lengo letu ni kutaka kuona ligi yetu ikipanda viwango vya ubora na wachezaji wakipata soko nje ya nchi ili kuvutia wawekezaji zaidi, na hilo haliwezi kutokea kama waamuzi wanaovurunda wataendelea kufumbiwa macho. Katika hilo, ni vema pia TFF na TPLB ikamulika maslahi yao kwa mapana zaidi ili kuwapunguzia kuingia vishawishini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Makaka ana 'vitu vingi' vya Mwameja

Na Adam Fungamwango

**TAYARI** mashabiki wa soka nchini, watangazaji na wachambuzi wa michezo wameanza kumfuatilia kipa wa Ruvu Shooting, Mohamed Makaka kutokana na umahiri wake wa kudaka na kuokoa michomo au hatari langoni mwake kwa ustadi wa hali ya juu.

Makaka ameanza kuwa kivutio kwa wapenzi wengi wa soka na wadau, baada ya mechi mbili mfululizo za timu yake ya Ruvu Shooting dhidi ya timu kongwe za Simba na Yanga.

Pamoja na Ruvu Shooting kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Yanga Novemba 2, mwaka huu, lakini kipa huyo aligeuka kuwa shujaa kwenye mechi hiyo iliyoangaliwa na watu wengi.

Kuna baadhi ya watu waliona kama vile siku hiyo aliamka vizuri, aliamua kucheza vile kwa kuikamia Yanga, ikabidi wamwangalie tena kwenye mechi nyingine dhidi ya Simba, ambayo nayo mbali na kuokoa mkwaju wa penalti aliokoa hatari nyingi za wazi. Unaweza kusema mabao aliyofungwa Makaka yalikuwa mepesi zaidi kuliko yale aliyookoa. Mwisho wa siku Simba ilishinda 3-1 mechi iliyochezwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Novemba 19, mwaka huu, lakini Makaka akiwa shujaa.

Kwa bahati mbaya sana Jumamosi iliyopita, Makaka aliumia kwenye mechi ambayo Ruvu Shooting ilicheza dhidi ya Kagera Sugar alipokuwa akijaribu kuokoa shuti la juu lililopigwa umbali wa mita 18. Kuna baadhi ya watu kwenye vibanda umiza baada ya kipa huyo kuumia, wakaanza kuondoka.

Walipoulizwa kwa nini wanaondoka wakati mechi bado mbichi, wakasema wao walikuja kumwangalia Makaka, hivyo kama ameumia hawana tena hamu ya kuuangalia mchezo huo.

Baadhi ya watu wameanza kumpigia upatu achaguliwe kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, huku wengine wakiiona njia nyeupe kwa kipa huyo kutoka kwenye klabu hiyo na kwenda nyingine kubwa kuliko hiyo na hasa klabu zenye uchumi mkubwa ambazo ni Simba, Yanga na Azam FC.

Siyo kipa mpya kwenye Ligi Kuu, kwani aliichezea Stand United wakati ikicheza Ligi Daraja la Tatu hadi ikiwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa nini Makaka kwa sasa amekuwa kivutio kwa mashabiki wengi? Kwa nini amekuwa akiokoa hatari nyingi au mabao ya wazi. Nilichokigundua kuwa Makaka ana uwezo mkubwa wa kuruka 'diving', kuliko makipa wengi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kama siyo wote.

Ana uwezo wa kuruka kutoka upande mmoja kwenda mwingine, miguu ikiwa hewani, lakini ana uwezo wa kuruka kwenda juu akiwa amenyooka au amepinda.

Mfano, kwenye mechi dhidi ya Simba aliokoa mabao mawili, moja ni faulo ya Bernard Morrison na shuti la Denis Kibu akiwa ameruka hewani, huku akiwa amejikunja kama samaki aina na mkizi. Hizi ndizo staili za makipa wa kizamani, na huwezi kuzipata kwa makipa wa kisasa.

Ndiyo maana hata mashabiki wamekuwa wakipenda kumtazama kwa sababu wanaonekana kuburudika kwa jinsi anavyookoa baadhi ya michomo kwa staili hiyo.

Baadhi ya mashabiki wa soka wa zamani wanadai wakati mwingine huwa wanakwenda uwanjani kwa ajili ya kuangalia baadhi ya wachezaji jinsi wanavyocheza, kwani wanaburudisha. Hivyo ndivyo makipa na baadhi ya wachezaji wa zamani walivyokuwa.

Makipa wa sasa ni wazuri, lakini wanadaka zaidi kwa 'timing', lakini wanapotea, ingekuwa ngumu zaidi kuokoa hatari zaidi ya kufungwa. Unakuta kipa anasimama tu. Kipa kama Makaka mwenye uwezo wa kuruka, anaweza kujikunjua na kuokoa hatari ambayo tayari alikuwa ameshapotea maboya.

Hivi ndivyo makipa wa zamani kina Mohamed Mwameja, Idd Pazi, Kichochi Lemba, Juma Pondamali, Omari Mahadhi, Ahumani Mambosasa, Hamisi Kinye, Joseph Fungo, Mahmood Nyalusi, Dan Poka, Mkala Mauli-di, Paul Rwechungura, Madata Lubigisa, na wengineo wengi walikuwa wakifanya.

Zamani sifa namba moja ya kipa ilikuwa ni lazima ujue kuruka au kuchumpa, kulia, kushoto, juu, na kunyumbulika. Halafu siri nyingine ni kwamba baadhi ya makipa wengi wa zamani walikuwa wana uwezo mkubwa wa kucheza sarakasi au walicheza mchezo huo wakiwa wadogo, na hii iliwasaidia sana kwenye kazi hiyo hasa kwenye eneo la 'diving'.

Ndiyo maana hata mimi nikimwangalia Makaka, ananikumbusha makipa wale wa zamani walivyokuwa wakilitawala goli kutokana na uwezo mkubwa wa kudaka, kuruka, na kuokoa michomo kwa ustadi, huku wakiongeza na mbwembwe, na mikogo kibao.

Niliwahi kuzungumza na kipa Doyi Moke aliyechezea klabu za Simba na Yanga, akasema makipa wa zamani hawakuwa wanapenda kukaa golini bila kushambuliwa. Huwa wanapenda wapinzani hao washambulie na kupiga mashuti ili naye aonyeshe umahiri wa kudaka na kuruka kama nyani, aonekane na kushangiliwa na mashabiki. Tumpe muda Makaka anaweza kuleta kitu tofauti kwa makipa vijana wanaochipukia, kwani wanaweza kuiga aina yake ya udakaji hasa kwenye staili ile ya 'diving' inayomsaidia sana kuokoa mabao mengi ya wazi, akiwashinda makipa mengi mahiri wenye majina makubwa, ambao kwao 'diving' ni shida.

HABARI KITAIFA

# Wawekezaji Oman waonyesha nia kununua nyama, mifugo

Na Mbaraka Kambona

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema wizara yake itaendelea kuweka mazingira wezeshi yatakayowavutia wawekezaji katika sekta ya mifugo, ili kukuza thamani ya mifugo na kupandisha kipato cha wafugaji nchini.

Ndaki aliyasema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki alipokutana na wawekezaji kutoka Oman ambao wameonyesha nia ya kufanyabiashara ya kununua mifugo na nyama nchini na kuuza nchini Oman.

"Tunaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kadri iwezekanavyo ili muweze kufanya hiyo biashara na nchi yetu," Ndaki aliwaeleza wawekezaji hao.

Alisema kuwa nchi ikipata wawekezaji kutoka nje kama wao ni jambo jema kwa sababu kupitia wao wafugaji watapata kipato kizuri, lakini itapandisha thamani ya mifugo nchini.

"Tukipata soko la kwenu litasababisha wafugaji wetu ambao wengi wao kipato chao kipo chini kiweze kupanda, sisi tutafanya kila linalowezekana ili biashara hii mnayotaka kuifanya iweze kufanikiwa," alisisitiza.

Awali, Mkurugenzi wa Kampuni ya Desert Cold Store kutoka Oman, Dk. Munawar Pardhan, alisema lengo lao ni kufanya biashara ya mifugo na nyama, huku akisema kuwa wakifanikiwa itakuwa ni fursa kubwa ya kiuchumi kati ya nchi hizo mbili.

"Tumekuja Tanzania kujua taratibu za kufuata ili tuweze kufanya biashara ya mifugo na nyama kutoka hapa na kwenda kuuza Oman," alifafanua Pardhan.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC), Balozi Patricia Danzi (wa pili kushoto) akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki pamoja na Mkuu wa SDC, Mashariki na Kusini mwa Afrika, Peter Bieler (kushoto).
**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Lukuvi awanyooshea kidole watendaji

Na Mary Geofrey

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema watendaji wa sekta mbalimbali za wizara hiyo wamekuwa sehemu ya changamoto za ardhi ikiwamo upimaji na urasimishaji.

Lukuvi aliyaeleza hayo mwishoni mwa wiki, mkoani Dar es Salaam, wakati akifungua kongamano la siku mbili la wapima ardhi la mwaka 2021.

Kongamano hilo lililenga kubadilishana mawazo na kujadili changamoto zinazowakabili katika sekta hiyo, chini ya kauli mbiu inayosema; 'Jukumu la taaluma ya upimaji ardhi katika ujenzi wa miundombinu na maendeleo endelevu'.

Aliwataka wapima ardhi nchini, kujitathmini na kujisafisha kwa sifa mbaya walizonazo kwa kujitangaza badala ya kuendelea kukaa kimya ilhali sekta hiyo ina sifa njema.

"Yale mazuri mengi mnayofanya myatangaze ili watu wayatambue na mchango wenu ujulikane kwa jamii, badala ya kujifungia na kuendelea kufanya madudu," alisisitiza Lukuvi.

Aidha, aliwataka watendaji hao kuwaripoti maofisa ardhi wanaofanya kazi za kuitapeli ili watambuliwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Alisema ili kumaliza changamoto hizo mwakani ataandaa wiki moja ya ardhi ili kuwakutanisha pamoja wadau wote wa sekta hiyo, kutoka serikalini na sekta binafsi.

Alisema mkutano huo utasaidia kutoa malalamiko na changamoto zao ili kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu. Kadhalika alisema serikali imetoa Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kupima halmashauri na wilaya zote nchini.

Aidha, alisema kuna mradi mkubwa wa kupima na kupanga maeneo yote nchini, ambao utasaidia kuboresha halmashauri.

Aliwataka wanataaluma hiyo kuchangamkia fursa hiyo ya kupima ardhi ili kusaidia serikali kumalizana na changamoto ya migogoro ya ardhi nchini.

# Uswisi kujengea uwezo Watanzania ujasiriamali

Na Christina Mwakangale

SERIKALI ya Uswisi imesema imelenga kuwajengea uwezo Watanzania, hususan vijana, kuimarisha mafunzo, shughuli za taasisi na ujasiriamali, ili kuinua kiwango cha maisha cha kundi hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC), Balozi Patricia Danzi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam, kuhusu ushirikiano wa miaka 40, baina ya Tanzania na Uswisi.

Alisema, Waswisi wapo tayari kuja kuwekeza Tanzania kwenye miradi tofauti, ikiwa kuna sera na sheria zinazowahakikishia uwekezaji wao na kwamba mpango wa nchi yake hapa nchini, 2021/24 umelenga kuwezesha ujasiriamali, huduma za afya, elimu ya uraia na mabadiliko ya tabianchi.

"Niwahakikishie kwamba Tanzania itapokea wawekezaji kutoka Uswisi, na kufungua fursa kwa vijana, hasa katika mafunzo ya elimu ya ufundi," alisema Balozi Danzi.

Mkuu wa SDC, Mashariki na Kusini mwa Afrika, Peter Bieler, alisema mpango huo wa miaka minne utazingatia kuimarisha shughuli za kujipatia kipato kwa uchumi endelevu.

"Kuimarisha mtazamo wa wajasiriamali na kujikita kwenye biashara endelevu ni muhimu kwa kizazi kijacho," Bieler.

Aidha, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alishuhudia uzinduzi wa mpango huo wa miaka minne wa nchi mbili, akisema Tanzania inajivunia uhusiano mzuri na Uswisi kwa miongo kadhaa.

Mulamula alisema Uswisi imeendelea kuwa kati ya nchi zilizo kati ya wadau wa maendeleo wa Tanzania, kuimarisha uchumi unaojumuisha jamii na kupunguza umaskini katika mikoa iliyo chini kiuchumi, akisema Tanzania imekwishapokea dola bilioni moja kutoka Uswisi kwa kipindi cha miaka 40.

Kadhalika, Mulamula alisema, serikali ipo katika hatua za mwisho kuifanyia marejeo sera ya uwekezaji ya mwaka 1996, ili iwe shirikishi na kuihisisha sekta binafsi.

# Wananchi walalamika kuuziwa kadi za kliniki

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

MBUNGE wa Jimbo la Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, ameiomba serikali kuingilia kati suala la wananchi kuuziwa kadi za kliniki katika zahanati ya Boko Mnemela, utaratibu ambao unadaiwa kufanyika kwenye steshenari iliyopo karibu na zahanati hiyo.

Mwakamo alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa wananchi wa kijiji cha Boko Mnemela, kwa mama wajawazito kutoa malalamiko ya kadi zao kushikiliwa.

Aliahidi kumtafuta Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya kueleza sababu za wananchi hao kuuziwa kadi za kliniki utaratibu ambao hautambuliki serikalini.

"Hapa kuna shida ya usimamizi, utaratibu ni kwamba kadi zikiisha inatolewa taarifa kwenye ngazi husika na sio kuanza kuuziana kadi kwa kinamama wajawazito na hii siwezi kulivumilia liendelee," alisema.

Mmoja wa wakazi wa Boko Mnemela, Diana Simon, alikiri kuwapo kwa hali hiyo na kwamba wakati wa kununua kadi hizo zipo za kutoa nakala ambazo nyepesi ni Sh. 100 na nzito ambayo itadumu kwa muda ni Sh.1,000.

Naye Sada Msumi alisema zahanati hiyo ina kero nyingi kwa upande wa wajawazito kwa kuwa chumba cha kujifungulia ni kidogo chenye uwezo wa kuhudumia mtu mmoja pekee.

Aidha, John Dotto alimwomba mbunge huyo kusimamia upatikanaji wa kituo cha afya katika kata hiyo kutokana na huduma nyingi zinazotolewa katika zahanati hiyo hazikidhi mahitaji ya wagonjwa na kuwalazimu wakati mwingine kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya katika kituo cha afya mkoani.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Boko Mnemela, Jumanne Msusa, alisema kutokana na ufinyu wa baadhi ya vyumba katika zahanati hiyo serikali ilitoa Sh. milioni 19.3 kwa ajili ya ukarabati, lakini walishangazwa na kitendo cha fedha hizo kupelekwa kwenye ujenzi wa choo cha zahanati ambacho hakikuwa kipaumbele.

Msusa aliiomba serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza vyumba vya kujifungulia kwenye zahanati hiyo kuondoa kero iliyopo. Akizungumzia tuhuma za kadi Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Boko Mnemela, Dk. Agnes Lutema, alikiri kukosekana kwa kadi katika zahanati hiyo.

Alisema kwa muda mrefu hawajaletewa kadi kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) hali inayowalazimu kutoa kadi iliyopo kwa kinamama wakatoe kopi ili waendelee na huduma badala ya kutumia madaftari ambayo yanachakaa mapema.

"Hatuuzi kadi kwenye zahanati yetu hapa akija mtu anahitaji kuanza huduma ya kliniki tunampa aende akatoe kopi hatumpangii wapi pakutolea hakuna maslahi yoyote kwenye steshenari tunafanya hivyo ili waendelee na huduma wakati tunasubiri kuletewa kadi nyingine," alifafanua.

Aidha, alibainisha kuwa suala la kiwango cha gharama za kadi inategemea na anayeenda kutoa nakala anataka ya aina gani ngumu au nyepesi na gharama zake zinatofautiana.



Mratibu Mkuu wa Taasisi ya Omuka Hub, Lovelet Lwakatare, akitoa ufafanuzi kwa baadhi ya washiriki waliofika katika maonyesho ya zana za kidigitali ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MORAJI MSALA**

# Kafulila 'awawakia' MaDED miradi UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amewataka wakurugenzi watendaji wa halmashauri za Itilima na Maswa kujieleza kuchelewesha utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa madarasa kwa fedha za UVIKO-19.

Kafulila alitoa agizo hilo kupitia Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, wakati akifunga kongamano kujadili namna ya kurejesha ushirika wenye nguvu mkoani humo.

"Wakurugenzi wa Maswa na Itilima nataka maelezo ya maandishi kwanini ujenzi kuwa chini ya asilimia 10 mpaka sasa ni jambo lisiloingia akilini," alisema.

Hata hivyo, alizipongeza halmashauri za Bariadi mjini na vijijini waliofikia asilimia 90, Meatu asilimia 72 na kuwaweka kiporo Busega waliofikia asilimia 36.

Aidha, ameelekeza wakurugenzi na wakuu wa wilaya kufunga taa na ujenzi kuendelea usiku na mchana, ili kuhakikisha Desemba 15, mwaka huu madarasa yanakabidhiwa na wanafunzi waanze kuyatumia.

Katika hatua nyingine, Kafulila aliwataka watendaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo kujitathmini utendaji wao kwa kuzingatia kilio cha wananchi cha rushwa hasa kwenye vyama vya ushirika.

Alisema changamoto kubwa iliyobainishwa ikiwa ni rushwa na dhuluma wanayofanya baadhi ya viongozi wa vyama vya msingi- AMCOS wakati wa mauzo wanamlipa mkulima bei pungufu tofauti na waliyopokea toka kwa mnunuzi.

"Nimekwishaelekeza mara kadhaa TAKUKURU mfanye uchunguzi nijue AMCOS zipi ambazo kiasi zilichopokea kwa mnunuzi ni tofauti na kiasi ilichomlipa mkulima. Sijui mnataka kuwa sayansi gani kujua ukweli huu wakati mauzo yote yanafanyika kwa nyaraka," alisema. "Haiwezekani kila mmoja kuanzia ukumbini hapa na hata mtaani tunajua mchezo huo ulifanyika lakini mamlaka ya TAKUKURU mnavuta miguu kuweka ukweli kilichotokea.

"Sasa tangu niseme jambo hili Oktoba mwaka huu msimu ulipokwisha na hadi leo hamjaleta taarifa basi ikifika mwisho wa mwezi huu nijue mbivu na mbichi," alisema na kuongeza;

"Kama sayansi ya kutafuta ukweli wa jambo wazi namna hii hamna basi itabidi mbadilike au nizijulishe mamlaka mbadilishwe kwa kushindwa kutimiza majukumu yenu, haiwezekani kila mtu analalamika."

# Jukwaa la uwezeshaji wanawake lashauriwa

**Na Munir Shemweta,** SHINYANGA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi mkoani Shinyanga kutumika kama nyenzo ya kuwaletea maendeleo sambamba na kuwahamasisha wanawake kuwa na umiliki wa ardhi.

Akizungumza na wanawake wa jukwaa hilo kutoka kata 17 za mkoa wa Shinyanga mwishoni mwa wiki mkoani humo, Dk. Mabula alisema kiu yake ni kuona majukwaa ya wanawake nchini yanafanya kazi ya kuwawezesha wanawake ikiwamo kumiliki ardhi hasa ikizingatiwa kuwa mwanamke ni nguzo ya maendeleo. "Tunachotaka sasa kama wanawake hatuwaachi nyuma wanaume lakini na sisi lazima tujiimarishe kiuchumi maana tumekuwa wasindikizaji kwa muda mrefu, tunataka kubadilisha ni kama tumechelewa," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Mabula, mwanamke akikamata uchumi maendeleo lazima yatakuwapo na kwa muda mrefu mwanamke amebaki nyuma wakati anaweza kufanya mambo makubwa na kuwataka wanawake kutoigana kwenye vitu vitakavyowashinda kuvisimamia.

Aidha, aliwataka wanawake hao wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Shinyanga kusimamia yale mambo waliyokubaliana na kuongeza kuwa, jukwaa lisipojiandaa katika shughuli zake itakuwa ngumu kufanikiwa.

"Kuna fursa katika maeneo yetu na tunahitaji mitaji mikubwa na tuwe na miradi itakayokuwa vielelezo na tusiende ili mradi tu bali tuwe na shughuli kubwa za uzalishaji mali, Roma haikujengwa kwa siku moja," alisema Dk. Mabula.

Kuhusu umiliki wa ardhi kwa wanawake, Mabula aliwataka wanawake kuanza kujitokeza kuomba umiliki wa ardhi hasa kwenye maeneo mapya sambamba na kuhakikisha ardhi wanayoipata iwe imepimwa. Aliwaambia kuwa sheria ya ardhi haizuii mwanamke kumiliki ardhi hivyo wachangamkie kupata ardhi katika maeneo mapya ya mkoa huo inapopita miradi ya kimkakati.

"Kwa sasa sisi wanawake lazima tubebe umiliki wa ardhi na kuitumia kijiletea maendeleo kama vile kuchukulia mikopo katika benki," alisema Mabula.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwataka wanawake wa mkoa huo kuanza michakato ya kuhakikisha nao wanamiliki ardhi ili kujiletea maendeleo.

# TAKUKURU yaagizwa tril. 1.3/- za miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais (Menejimenti na Utumishi wa Umma), Deogratius Ndejembi, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufuatilia kwa kina matumizi ya fedha za miradi ya Sh. trilioni 1.3 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo.

Ndejembi aliyasema hayo wakati akifungua mkutano mkuu wa TAKUKURU wa kufanya tathmini ya utendaji kazi uliofanyika jijini Dodoma.

Alisema kumekuwa na harufu ya rushwa katika miradi hiyo, hivyo ni lazima wao wakafanye kazi yao kama serikali inavyowajali watumishi wa taasisi hiyo.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha hizo ili miradi ya wananchi iweze kutekelezwa kikamilifu na kuleta manufaa kwa jamii nzima.

"Nahitaji kuona mnaifuatilia miradi hii sio kukaa ofisini tu, kinachotakiwa mkatende kazi mliokabidhiwa," alisema Ndejembi.

Alisema lengo la serikali ni kuona kila mradi ambao unatekelezwa unakamilika bila vikwazo vyovyote ili wananchi waanze kuutumia.

Alisema miradi hiyo inatekelezwa nchi nzima, hivyo nao mkutano huo ujitathmini wakaufanyie kazi ili kufuatilia fedha hizo kwa umakini.

Aliipongeza taasisi hiyo kutokana na utendaji kazi na kuitaka kutobweteka, badala yake wafanye kazi kwa bidii ili kuisaidia serikali. Alisema taasisi hiyo inaheshimika, hivyo nao wazidi kuwaaminisha wananchi kwa utendaji ambao wanaendelea kuuonyesha kwa wananchi.

"Tayari tumepandisha madaraja watumishi wakiwamo wa TAKUKURU, tutaendelea na zoezi hili, hatujafikia mwisho," alisema Ndejembi.

Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Kamishna wa Polisi Salum Hamdun, aliwataka watumishi kuendelea kuchapa kazi baada ya mkutano huo ili waendelee kulipa sifa taifa na taasisi hiyo.

Aliwataka kwenda kuyafanyia kazi yale waliyojadili katika mku-



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiriba Halmashauri ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara sambamba na wafanyakazi wa Benki ya NBC tawi la Musoma na uongozi wa shule hiyo, wakionyesha sehemu ya msaada wa mifuko 920 ya saruji iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa mabweni mawili katika shule hiyo, wakati wa hafla ya makabidhiano iliyofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mara na Mtwara yapigwa jeki kwa elimu

**Na Mwandishi Wetu**

MIKOA ya Mara na Mtwara imepigwa jeki katika sekta ya elimu kwa kupatiwa msaada wa mifuko ya saruji 920 (sawa na tani 46) yenye thamani ya Sh. milioni 21 pamoja na madawati 100.

Msaada huo umetolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ambapo saruji hiyo ni kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili katika shule ya sekondari Kiriba iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara sambamba na msaada wa madawati 100 katika shule za Sekondari Libobe na Tangazo zilizopo mkoani Mtwara ikiwa ni hatua ya benki hiyo katika kuunga mkono juhudi za serikali pamoja na wananchi katika kuboresha elimu nchini.

Wakizungumza kwenye hafla za kukabidhi misaada hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki katika shule hizo, Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Musoma, Sophia Lyimo pamoja Meneja wa benki hiyo tawi la Mtwara, Editha Mwakatobe, walisema misaada hiyo inalenga kuunga mkono jitihada ambazo tayari zinaendelea kuonyeshwa na serikali pamoja na wananchi katika maeneo husika kwa kuboresha miundombinu ya elimu.

"Mifuko hii 920 ya saruji tunayoikabidhi hii leo ni kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa mabweni mawili ya wasichana na wavulana katika Shule hii ya Sekondari Kiriba. Wananchi na serikali wamefanikisha ujenzi wa maboma ya mabweni na sisi tumeona tuwaunge mkono kwa kuwapatia saruji ili waweze kufanikisha mpango huu muhimu unaolenga kuwasaidia wanafunzi wanaosoma hapa wasitembee umbali mrefu kufuata elimu," alisema Lyimo.

Aliipongeza serikali kwa kutoa kiasi cha Sh. milioni 60 kufanikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo.

Akizungumza kwenye hafla kama hiyo ya kukabidhi madawati 50 kwa ajili ya shule ya sekondari ya Libobe iliyopo wilayani Mtwara, Meneja wa Benki ya NBC tawi la Mtwara, Mwakatobe alisema msaada ni sehemu ya msaada wa madawati 100 unaotolewa na benki hiyo kwa shule hiyo ya Sekondari pamoja na sekondari ya Tangazo iliyopo wilayani humo pia, lengo likiwa ni hilo la kuhakikisha wanasaidiana na serikali pamoja na wananchi katika kuboresha mazingira ya elimu nchini.

"Lengo letu ni kuhakikisha ndoto za watoto hawa kielimu zinafikiwa na pia kumuunga mkono Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, katika utoaji wa elimu bora.

Kwa hiyo tunakabidhi madawati na viti hivi kwa ajili ya wanafunzi hawa kwa kuwa ni furaha ya NBC kuona watoto wanaondokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili hasa katika suala la elimu," alisema Mwakatobe.

Akizungumza baada ya kupokea msaada wa viti na madawati kwa ajili ya Sekondari ya Lipobe, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya pamoja na kuishukuru benki hiyo kwa msaada huo, alisema serikali imejipanga kuhakikisha inamaliza changamoto za kielimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo benki hiyo huku akitolea mfano shule hiyo ambayo inaendelea na ujenzi wa madarasa mawili na ofisi ya walimu kupitia fedha kiasi cha sh mil 40 zilizotolewa na serikali.

"Msaada huu umekuja wakati muafaka kwa sababu mahitaji ni viti na meza 72 kwa ajili ya wanafunzi watakaonza masomo mapema mwakani...tunawashukuru sana benki ya NBC kwa kutuunga mkono baada ya kuwapelekea maombi yetu na wao hawakusita kutusaidia."

Kwa upande wao wakuu wa shule hizo waliishukuru benki hiyo kwa namna ilivyoguswa katika kuchangia sekta ya elimu ikiwamo ujenzi na ukarabati wa vyumba vya madarasa, mabweni na msaada wa madawati kwa kuwa jitihada hizo zimekuwa zikisaidia kuongeza kasi ya serikali na wanachi wanaojitolea kuboresha utoaji wa elimu hapa nchini.

"Binafsi nimefarijika sana kwa msaada huu kutoka NBC na kwa kweli bado tunahitaji wadau wengine wajitoe kusaidia kama walivyofanya benki hii. Tulituma maandiko ya kuomba msaada kwao na tunashukuru waliyapokea na kuyafanyia kazi na matokeo yake ndio haya tunayaona hii leo tunapokea msaada huu mkubwa wakilenga kuunga mkono jitihada za wananchi na serikali yetu," alisema Mtani Shadrack, Mkuu wa Shule ya Sekondari Kiriba, wilayani Musoma.

## Wanafunzi elimu ya juu kushindana insha

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limezindua shindano la insha kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini katika kuelekea Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Viwango Afrika (ARSO) ambayo yatafanyika Machi mwakani.

Uzinduzi wa shindano hilo ulifanywa mwishoni mwa wiki kwenye Makao Makuu ya shirika hilo jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Shirika hilo, Mhandisi Johaness Maganga, akisema kila mwaka ARSO huidhinisha maudhui ya insha na hualika mashirika ya viwango barani Afrika kuandaa shindano la insha kwa vyuo vikuu ngazi ya kitaifa.

Kwa mujibu wa Maganga, washindi watano watakaopatikana katika kila nchi wanashindanishwa katika ngazi ya Afrika. Kwa upande wa mshindi wa kwanza katika ngazi ya Afrika atapata fursa ya kushiriki mkutano mkuu wa ARSO utakaofanyika Cameroon mwezi Juni mwakani.

Mhandisi Maganga alisema kwa Taanzania, TBS huratibu shindano hilo katika ngazi ya Taifa, ambayo inahusisha kutoa matangazo kwa wanafunzi kushiriki, kupokea insha kutoka kwa washiriki na kutoa washindi.

Alisema wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu watashiriki na kuandika insha kuhusu kauli mbiu ya mwaka huu isemayo "Jukumu la Viwango katika kukuza sekta ya dawa na vifaa tiba Afrika, kufikia kujitegemea na ustahimilivu katika mapambano ya Uviko-19 na magonjwa mengine ya mlipuko wakati ujao."

Kwa mujibu wa Maganga, uandishi wa insha unalenga kuwawezesha vijana wa Kiafrika kuelewa umuhimu wa viwango katika kuwezesha maendeleo endelevu barani Afrika.

Meneja Viwango wa TBS, Nasra Husein, alisema kauli mbiu ya mwaka huu, inasisitiza maendeleo endelevu ambayo yanalenga kushughulikia usawa kwenye jamii na kukuza uchumi endelevu na kupunguza kasi ya mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema ili kuyafikia malengo hayo inahitajika ushirikiano wa mashirika ya umma na binafsi na matumizi ya zana zote zilizopo ikiwa ni pamoja na viwango vya kimataifa na udhibiti ubora.

## Wanaowadharau walimu waonywa

Na Elizabeth John, NJOMBE

KATIBU Tawala Wilaya ya Njombe, Emmanuel George, amesema jamii inapaswa kuondoa dhana potofu iliyojengeka kwa watu wengi kuhusu taaluma ya ualimu kwamba ni ya watu waliofeli.

Aliyasema hayo katika semina elekezi ya kuwajengea uelewa wa kimaadili walimu wa shule za msingi na sekondari iliyoandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Njombe, ambapo alisema walimu sio wito bali ni taaluma inasomewa.

"Wito unatoka wapi? Daktari anasoma kwa sababu anaenda kuhudumia wagonjwa, hii ni taaluma kama taaluma nyingine," alisema George.

Aliongeza: "Fani ya ualimu sio kimbilio la waliofeli darasani, lazima iheshimiwe, hii ni taaluma ambayo haipaswi kudharauliwa, nawaomba sana walimu waheshimiwe ili watuandalie kizazi kilicho bora."

Pia alikemea suala la maadili kwa walimu katika mavazi; "Walimu hatuzingatii maadili ya kazi, uvaaji wetu, mawasiliano ya lugha tunaongea vibaya mitaani hadi shuleni, wakati mwingine unakuta hata soksi hajavaa wanasema ndio mikato ya sasa hivi yaani tunavyovaa na kuongea hatuendani na uhalisia," alisema George.

Wakizungumza baada ya semina hiyo, baadhi ya walimu wameipinga kauli ya kwamba walimu ni kichaka cha waliofeli darasani, na kwamba jamii inapaswa kuondoa dhana potofu.

"Mimi kauli hii naikataa uwalimu ni kazi kama kazi nyingine ni fani ambayo unapaswa kuingia darasani ndio maana kwa hawa hawa walimu kuna wenye shahada, astashahada na kuendelea, hata mishahara tuko sawa ngazi moja," alisema Angelina Matumika.

Naye Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Njombe, Varian Ngalioma, alisema walimu wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo za kimazingira.

"Mazingira kwa maana ya kutotimiziwa stahiki zao pia wakati mwingine kwa kukosa vifaa na vitendea kazi mbalimbali kwa hiyo mazingira ndio yanasababisha hii tasnia yetu, idara yetu ya ualimu kuwa na changamoto," alisema Ngalioma.

# Wanaharakati waona mfumo dume uongozi vyama vya siasa

Na Yasmin Protace

VIONGOZI wanawake kutoka vyama 19 vya siasa nchini, wamesema mfumo dume uliopo katika baadhi ya vyama umekuwa ukimkandamiza mwanamke ikiwamo kutopata fursa ya ushiriki katika uamuzi.

Hayo yalisemwa na baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kwa nyakati tofauti, walipokuwa katika mafunzo ya siku tatu yaliyolenga mada isemayo umuhimu wa utekelezaji wa masuala ya kijinsia katika vyama vya siasa.

Mafunzo hayo ambayo yaliratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kushirikiana na Ulingo, baadhi ya viongozi wa vyama hivyo walisema kwa nyakati tofauti mfumo dume uliopo katika vyama hivyo unachangia wanawake kushindwa kupata nafasi za juu upande wa katibu au mwenyekiti.

Walisema mfumo dume uliopo katika baadhi ya vyama unachangia hata wanawake kukosa nafasi ya ushiriki katika uamuzi.

Wameiomba Ofisi ya Msajili wa Vyama kabla ya kutoa usajili katika vyama waonyeshe kwanza katiba za chama kama zinamthamini mwanamke. Dk. Ave Maria Semakafu, Mratibu wa Taifa Ulingo, alisema chama chochote cha siasa kinachosajiliwa, lazima kizingatie masuala ya kijinsia. "Pamoja na kuwapo kwa sheria hiyo, lakini bado baadhi ya vyama viongozi wa juu ni wanaume hakuna mwanamke, hali hiyo inachangia haya wanawake kushindwa kufanya maamuzi," alisema.

Aliongeza kuwa kuna kipengele katika katiba kinasema binadamu wote ni sawa, lakini katika hilo la usawa katika vyama linaonekana halipo. Lilian Liundi, Mkurugenzi Mtendaji TGNP Mtandao, alisema wapo katika kutafakari kama viongozi wanawake uwakilishi wao katika ngazi za uongozi umeongezeka au bado haujafikiwa..

Aliongeza kuwa inatakiwa kuwapo na uwakilishi wanawake katika uongozi na kwamba ilani zinasema 50 kwa 50, lakini ilani haisaidii chochote kutokana na kuwapo kwa mapengo.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohamed Ally Ahmed, alisema mafanikio ya usawa wa kijinsia Tanzania yatatokana na wanawake kupambana wenyewe.

Aliongeza kuwa katiba inasema binadamu wote ni sawa na kwamba sheria ya vyama vya siasa inasema vyama vyote vya siasa viangalie usawa wa kijinsia.

"Sheria iboreshwe ili kuelekeza vyama vinatambua mwanamke katika nafasi za juu za uongozi," alisema na kuongeza kuwa kinachotakiwa ni kupambana na masuala ya kijinsia ili kuleta usawa.



Waziri wa Uwekezaji, Geofrey Mwambe (katikati), akisikiliza maelezo ya shughuli za utendaji za mgodi wa Barrick wa Bulyanhulu alipofanya ziara kwenye mgodi huo, wiki iliyopita, wengine ni maofisa waandamizi wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGACHA WETU**

# Waziri: Wahitimu elimu ya juu lipeni madeni

Na Christina Mwakangale

SERIKALI imewashauri wahitimu elimu ya juu, kujenga tabia ya kulipa madeni hususani mikopo ya elimu ya juu.

Imewaambia kuwa dawa ya deni ni kulipa, ikisisisitiza wawe na utamaduni wa kujiajiri ili kujipatia kipato badala ya kusubiri kuajiriwa serikalini.

Imesema ongezeko la usajili wa wanafunzi shule za msingi, elimu bure na wahitimu sekondari kuongezeka kutoka milioni 2.6 mwaka 2016 hadi milioni 2.3 mwaka 2020, kumesababisha mahitaji ya mkopo wanaojiunga na vyuo kuongezeka.

Akimwakilisha mgeni rasmi, Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, kwenye mahafali ya 47 ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), kwa wahitimu 3,766 waliofuzu fani za biashara, uhasibu, fedha na benki, bima na hifadhi ya jamii ikiwamo mifumo ya habari.

Kigahe, alisema wahitimu hao pia wajiandae kujiajiri na si kusubiri ajira serikalini, kuwa wabunifu, kuitegemea sekta binafsi na kuwa na mbinu za kitaaluma ambazo zinakabiliana na ushindani wa soko.

"Mikopo lazima iwe endelevu, ili kukamilisha ndoto za wengine na walionufaika na mkopo wakumbuke kulipa...huo utakuwa utamaduni mzuri kwa kutambua kuwa dawa ya deni ni kulipa.

"Nawaasa wahitimu kwamba huu ni mwanzo wa kwenda kuishi maisha. Mnaachana na ulimwengu wa nadharia mmeingia katika vitendo, lazima mfahamu namna ya kutatua matatizo, muache kufanya kazi kwa mazoea na mkawe wazalendo.

"Chuo hiki ambacho nami nimesoma, ni mchango mkubwa katika sekta ya fedha, juhudi zinahitajika, kuimarisha weledi, utafiti kuisaidia serikali kukabiliana na changamoto za kiuchumi," alisema Kigahe.

Awali, Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Immanuel Mnzava, alisema tangu chuo kuanzishwa mwaka 1972 kimefanikiwa kuongeza idadi ya kozi zilizokuwa mbili, benki na bima, Sasa zikiwa 34, huku wahitimu wapatao 70 na kufikia 14,305.

Alisema pamoja na mafanikio, kuna changamoto ikiwamo ufinyu wa madarasa, mabweni, hasa kampasi ya Dar es Salaam na kuiomba serikali kukiongezea majengo pamoja na wakufunzi chuo hicho.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema, alisema ongezeko la wahitimu kidato cha nne na sita, kumeongeza udahili wa wanavyuo, hivyo IFM ina mpango wa kujenga kampasi zingine Dodoma na Geita.

Nipashe
Spotika




CHAMA NA NJIA YA MAPRO 7 WALIONDOKA NA KUREJEA? UK. 14



Ronaldo



Virat Kohli



Messi

# NYOTA WA5 WANAOINGIZA FEDHA NYINGI INSTAGRAM

**LONDON, England**

KWA sasa Instagram imekuwa zaidi ya jukwaa lingine la mitandao ya kijamii. Facebook (sasa Meta) imevunja vizuizi vyote vya kimataifa na vya umri kwa kumuunganisha kila mtu. Uchunguzi unaonyesha kuwa kwa wastani, mtumiaji wa Instagram hutumia kama dakika 28 juu yake.

Vile vile imefungua njia kwa bidhaa na makampuni makubwa hadi madogo kuwezesha watu kuzifikia. Instagram pia ni mahali ambapo watu mashuhuri hutumia zaidi na mashabiki wao na kupata maoni ya maisha ya kila siku ya nyota wao.

Kuanzia nyota wa filamu hadi kwa wanamichezo, karibu kila mtu hutumia Instagram kwani inachukuliwa kuwa njia bora zaidi. Licha ya kuungana na mashabiki na kuchapisha kuhusu maisha yao ya kila siku, watu mashuhuri pia hupata malipo mazuri kwa machapisho yao.

Makala haya inawachambua wanamichezo watano wanaolipwa fedha nyingi zaidi kwa chapisho moja kwenye Instagram, hawa hapa...

**#5. LeBron James (Mpira wa Kikapu) - Dola 474,000**

LeBron James maarufu kama Mfalme James ndiye mchezaji maarufu zaidi wa mpira wa kikapu nchini Marekani, NBA. Anajivunia zaidi ya wafuasi milioni 102 kwenye Instagram. Mpira wa Kikapu ni mchezo mzuri na hauna umaarufu mkubwa sana nje ya Marekani. Hata hivyo, haikuwa kikwazo kwa LeBron James kujulikana ulimwenguni kote.

Mzaliwa huyo wa Ohio, anaingiza takriban dola 474,000 kwa kila chapisho la Instagram. LeBron James anapata wafuasi wengi kwa mfumo wake wa mazoezi ya mwili.

**#4. Virat Kohli (Kriketi) - Dola 680,000**

Nahodha wa Timu ya Kriketi ya India, Virat Kohli anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote wa mchezo huo. Takwimu zake za kuvutia zinaambatana na sifa yake na hiyo inamfanya kuwa mmoja wa nyota wa michezo wanaofuatiliwa zaidi kwenye Instagram.

Kriketi, ukiwa ni mchezo mwingine mzuri, hauwezi kufurahiwa kama ilivyo kwa ule wa soka. Licha ya hayo, Virat Kohli anajivunia wafuasi wengi zaidi kuliko wanasoka wengi. Kohli ana wafuasi milioni 168 na ndiye mtu anayefuatiliwa zaidi nchini India.

**#3. Neymar Jr (Soka) - Dola 824,000**

Tangu akiwa kule Santos, Neymar Junior, mara zote amekuwa gumzo. Alianza kama mchezaji kijana mwenye maajabu na ujuzi wake wa kucheza katika ligi ya Brazil. Aliendelea kutawala Ulaya pamoja na Lionel Messi na Luis Suarez akiwa na Barcelona. Maisha ya Neymar yamezidi kukua na kuwa juu.

Umarufu zaidi ulikuja baada ya Mbrazil huyo kuhamia PSG kama mchezaji ghali zaidi katika historia ya soka. Alitua pale Paris mwaka 2017 kwa kitita cha euro milioni 222. Mashujaa wake wa ndani na nje ya uwanja wamemfanya Neymar kuwa mmoja wa nyota wa michezo wanaotazamwa zaidi kwenye sayari hii.

Pamoja na kuwa mwanasoka stadi, Neymar pia anachukuliwa kuwa mfano wa mitindo ya kisasa. Mitindo yake ya kunyoa nywele kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, imemfanya kuongeza umaarufu wake. Staili yake ya kuvaa pia huigwa na vijana wengi kote duniani. Neymar ana wafuasi milioni 165 kwenye Instagram na analipwa dola 824,000 kwa chapisho moja.

**#2. Lionel Messi (Soka) - Dola 1,169,000**

Lionel Messi na rekodi zinakwenda sambamba, si ndiyo? Katika ulimwengu huu wa kuvutia wa kandanda, raia huyo wa Argentina amejidhihirisha katika masuala ya ujuzi na fedha. Messi amebaki kuwa mmoja wa wanamichezo wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani.

Sehemu kubwa ya mapato yake hutokana na mishahara, mikataba binafsi na bila shaka, Instagram. Inaripotiwa kuwa nahodha huyo wa zamani wa Barcelona anaingiza takriban dola 1,169,000 kwa kila chapisho la Instagram na ana wafuasi milioni 281.

Ujuzi wa hali ya juu wa Messi na ushindani wake na Cristiano Ronaldo umemfanya kuwa mwanasoka maarufu zaidi wakati wote.

**#1. Cristiano Ronaldo (Soka) - Dola 1,604,000**


Akiwa na wafuasi milioni 367, Cristiano Ronaldo ndiye mtu anayefuatiliwa zaidi kwenye Instagram. Hahitaji utangulizi wowote ili kuhalalisha umaarufu wake mtandaoni. Ronaldo ndiye kielelezo cha utimamu wa mwili na akiwa na umri wa miaka 36, anacheza kama kijana wa miaka 22.

Vile vile humfanya kuwa mtu wa kuigwa kwa utimamu wa mwili na hivyo nahodha huyo wa Ureno amekuwa akifutiliwa sana na wapenda mazoezi. Chapa nyingi za kimataifa zimempata mwanasoka huyo wa zamani wa Real Madrid kama balozi wao, huku Nike ikiwa kinara.

Ronaldo anaishi maisha ya unyenyekevu nje ya uwanja na hutumia muda wake mwingi kuzunguka na familia yake. Chapisho la Ronaldo, ambalo alitangaza ujauzito wa mpenzi wake, ni chapisho la pili kupendwa zaidi kwenye Instagram.

## ISIKUPITE

LICHA ya kushindwa kuifunga Benfica kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa wiki iliyopita, Xavi Hernandez, amekuwa kocha wa 13 mfululizo kuepuka kipigo katika mchezo wake wa kwanza wa michuano hiyo kuiongoza Barcelona.



# CHAMA NA NJIA YA MAPRO 7 WALIONDOKA NA KUREJEA?

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa kumekuwa na habari nyingi zinazomhusu mchezaji wa zamani wa Simba, Clatous Chama kutaka kurejea nchini Tanzania, baada ya hali kuonekana kuwa tete kule Morocco akiwa na klabu yake ya RS Berkane.

Hakujawa na habari rasmi, lakini vyanzo mbalimbali vya habari, wakiwamo waandishi wa habari nchini Zambia na Morocco wanadai kuwa mchezaji huyo aliyesajiliwa na RS Berkane Agosti mwaka huu, akitokea Simba, hana furaha kwenye klabu hiyo na angetamani kurejea klabu yake hiyo ya zamani kipindi cha dirisha dogo, kwa sababu ndiyo timu ilimfanya kuwa mchezaji mkubwa, ikiwa na mashabiki ambao walimfanya aonekane kama mfalme.

Hata hivyo, vyanzo vingine vinadai kuwa wakala wake wanashinikiza mchezaji huyo arejee Tanzania, lakini kwenye klabu ya Yanga kwa sababu tayari ameongea nao, ingawa hilo linapingwa na mchezaji mwenyewe, aliyeonyesha mapenzi kwa Simba.

Iwapo mchezaji huyo raia wa Zambia atarejea kipindi cha dirisha dogo, ataungana na rundo la wachezaji wa kigeni ambao walicheza soka nchini Tanzania, wakaondoka kwa kuuzwa, au mkataba kumalizika, wakaenda wanakoenda na sasa wamekuwa wakirejea tena kukipiga hapa nchini, wafahamu...



Heritier Makambo

**#1. Heritier Makambo**

Amerejea tena kwenye klabu ya Yanga msimu huu. Ni mchezaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo anayecheza nafasi ya ushambuliaji. Awali alijiunga na klabu ya Yanga mwaka 2018 akitokea St Eloi Lupopo ya nchini Congo. Aliondoka nchini kwa kuuzwa na klabu yake nchini Guinea kwenye klabu ya Horoya mwaka 2019, lakini mwaka huu amerejea nchini Tanzania na kujiunga tena na klabu yake ile ile ya Yanga.

**#2. David Molinga**

Kwa sasa anaichezea klabu ya Namungo yenye maskani yake mkoani Lindi. David Molinga ambaye kama Makambo ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Alisajiliwa na Yanga mwaka 2019 kuziba nafasi ya Mkongomani mwenzake, Makambo kutoka kwenye klabu ya AC Lega ya nchini humo. Alidumu kwa msimu mmoja na kuondoka Tanzania kwenda kukipiga kwenye klabu ya Zesco ya Zambia. Kama ilivyokuwa kwa mwenzake Makambo, naye amerejea nchini msimu huu, lakini yeye akijiunga na Namungo, wote sasa wapo kwenye ligi moja.

**#3. Amissi Tambwe**

Ni straika ambaye ameshawahi kuwa mfungaji bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mara mbili msimu wa 2013/14 akiwa kwenye klabu ya Simba na 2015/16 akiwa na klabu ya Yanga. Hapa inaonyesha kuwa amezichezea klabu mbili kubwa nchini.

Simba ndiyo ilimleta nchini kwa mara ta kwanza, ikimsajili kutoka Vital'O ya Burundi. Straika huyo hatari raia wa Burundi aliichezea Simba msimu wa 2013 hadi 2014 akajiunga na Yanga, 2014 hadi 2019, alipoondoka nchini kwenda kuichezea Fanja ya nchini Oman. Msimu huu naye amerejea nchini. Anaichezea timu ya DTB inayocheza ngazi ya Championship ikisaka nafasi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao. Tambwe kwa sasa ndiye anaongoza kwenye ligi hiyo akiwa na mabao nane.

**#4. Nicolaus Gyan**

Naye pia sasa anaichezea Klabu ya DTB. Alikuwa ni mchezaji wa Simba kuanzia mwaka 2017 hadi 2019. Simba ilimsajili mchezaji huyo aliyekuwa akicheza nafasi ya ushambuliaji na baadaye kuwa beki wa kulia, kutoka Ebusua Dwarfs ya Ghana. Gyan, raia wa Ghana, aliondoka na kwenda kujiunga na klabu ya Legon Cities ya nchini kwao, lakini kwa sasa amerejea tena nchini kwenye klabu hiyo.

**#5. Tafadzwa Kutunyu**

Huyu ni kiungo mshambuliaji raia wa Zimbabwe, ambaye aliingia nchini mwaka 2017, akichezea klabu ya Singida United na baadaye kujiunga na Azam FC mwaka 2018. Mwaka mmoja baadaye aliondoka nchini kwenda Guinea kujiunga na klabu ya Horoya, lakini naye msimu huu amerejea nchini Tanzania na anaichezea DTB.


**#6. Papy Tshishimbi**

Pia kuna taarifa kwamba timu ya Kitayose inayoshiriki Championship, imemalizana na kiungo wa zamani wa Yanga Papy Tshishimbi. Mkurugenzi wa timu hiyo, Yusuph Kitumbo amethibitisha kumaliza na nyota huyo ambaye ataanza kutumikia baada ya dirisha dogo la usajili kufunguliwa. Naye atakuwa mchezaji wa nje, raia wa Jamhuri ya Congo anayerejea tena nchini.

**#7. Deo Kanda**

Pia Kutumbo amesema amemalizana na winga huyo wa zamani wa Simba, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kuichezea Kitayose inayoshiriki Championship, naye pia atakuwa mmoja wa wachezaji waliocheza nchini, na wakarejea tena kukipiga.

**JE, WAJUA?**



VIPIGO vitano vikubwa zaidi Lionel Messi alivyokumbana navyo katika wasifu wake kisoka; #5. Ligi ya Mabingwa 2018-19 (Liverpool 4-0 Barca), #4. Kombe la Dunia 2010 (Argentina 0-4 Ujerumani), #3. Ligi ya Mabingwa 2012-13 (Bayern Munich 4-0 Barca), #2. Kufuzu Kombe la Dunia 2010 (Bolivia 6-1 Argentina), Ligi ya Mabingwa 2019-20 (Barca 2-8 Bayern).







Aliyekuwa Mkurugenzi wa TAMWA, Ananilea Nkya (kulia), akimpongeza mjasiriamali katika kijiji cha Nronga Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Hellen Usiri baada ya kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Uzamivu (PhD) aliyotunukiwa na Chuo cha His Holy Word Biblia kwa kushirikiana na Chuo cha Corner Stone International Biblia kutoka Marekani kwenye mahafali yaliyofanyika Chuo Kikuu cha UDOM jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# BoT: Sera ya kuiwezesha sekta ya kilimo kifedha yaja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Yamungu Kayandabila, amesema wamejipanga kuja na sera ya kusaidia kifedha sekta ya kilimo ili kuiwezesha kutoa mchango wake katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Dk. Kayandabila alibainisha hayo juzi alipokuwa akifunga mkutano wa 20, wa Taasisi za Fedha nchini uliofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma.

Alisema BoT, hivi sasa inajipanga kuja na sera ya kusaidia kilimo katika utoaji wa mikopo ili kuwezesha sekta hiyo kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

"BoT imeamua kuliangalia eneo la kilimo na kuweka au kuja na sera ya kusaidia kilimo, tunaomba pia taasisi zingine za kifedha nchini kuliwezesha suala hili," alisema Dk. Kayandabila.

Alisema, taasisi za fedha nchini zinaweza kuja na bidhaa ambazo zitasaidia kilimo na wajasiriamali wadogo. "Lakini wanaweza kutumia teknolojia kuongeza kasi ya kutoa mikopo kwa mfano mikopo ya kwenye simu, pia kuwa na mikopo ambayo haita hitaji masharti magumu na ya muda mrefu," alisisitiza Dk. Kayandabila.

Alisema, BoT kwa kushirikia na Chama cha Taasisi za Fedha Tanzania (TBA) wataendelea kushirikiana kuongeza uwekezaji katika uchumi ili uendelee kufanya vizuri zaidi.

Aidha, alisema sekta ya kilimo nchini inayo nafasi kubwa katika kuchangia ukuaji wa uchumi hasa wakati huu ambao dunia imekumbwa na janga la UVIKO-19, kama itawezeshwa kikamilifu hasa katika suala la rasilimali fedha.

"Washiriki wa mkutano huu wa 20, wameeleza changamoto zilizopo kwenye kilimo, hivyo BoT imeamua kulingalia kwa upana suala hili na kuamua kuja na mikakati ya kukiwezesha kilimo chetu kuwa na tija hasa katika kufikia uchumi wa viwanda," aliongeza.

Vilevile, alisema elimu ya mikopo bado inahitajika kwa makundi mbalimbali yakiwamo ya wanawake, vijana na wajasiriamali wadogo ili watambue umuhimu wa kurejesha madeni yao kwa wakati. "Ni lazima watu wapate elimu ya mikopo ili kufahamu mkopo alioukopa una umuhimu gani na pia umuhimu wa kufanya marejesho ili kulipa deni la mkopo husika," alieleza.

Hata hivyo, alisema wataendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika utoaji wa mikopo ili kuiwezesha sekta ya kilimo nchini kupiga hatua na kuchangia katika ukuaji wa uchumi nchini.

# TBA na ZBA kutekeleza pamoja miradi Zanzibar

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Joseph Kilangi, amesema mpango uliopo kwa sasa ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kushirikiana na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) katika kutekeleza miradi mbalimbali visiwani humo.

Aidha, amesema ameridhishwa na miradi inayotekelezwa na TBA ambapo kupitia ZBA, na kwamba zimeahidi kufanya miradi yenye kiwango kama hicho.

Katibu huyo alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara ya ZBA kujifunza na kujionea miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa na TBA jijini Dodoma.

Miradi hiyo ni pamoja na ule wa Mji wa Kiserikali Mtumba awamu ya pili, mradi wa ujenzi wa nyumba 3,500 wa watumishi wa umma Nzuguni ambao umeanza na nyumba 150 na mradi wa ujenzi wa nyumba 20 za viongozi katika eneo la Kisasa.

Kilangi alisema kwa sasa wanaiamini TBA kwa asilimia 100, hivyo itashirikiana na ZBA kutekeleza miradi mbalimbali visiwani Zanzibar kwa lengo la kupata miradi yenye ubora kama Tanzania Bara. "Sasa mimi nadhani tuiamini TBA kwa asilimia 100 kama tunamiradi tutakayoianzisha basi TBA na wana miradi Zanzibar tutawaleta wataalamu wetu waje wafanye kazi kwa pamoja na TBA.

"Wazanzibar wategemee tutawaalika TBA Zanzibar, wategemee mambo mazuri hizi fedha tulizopata tuna shilingi bilioni 460 zinaenda mifukoni mwa watu kupitia miradi mbalimbali. Tutawaambia waje Zanzibar wasimamie miradi yetu," alisema.

Aidha, alisema mradi wa Mji wa Serikali awamu ya pili ni mzuri na utaonyesha kwamba Dodoma ni Makao Makuu ya serikali na ndoto ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere itakuwa imetimia kwa vitendo.

"TBA wamekuja na michoro mizuri na inajengwa kileo sana mazingira ni mazuri na vitendea kazi vimezingatia ubora, baada ya miaka miwili mitatu itaonekana kweli ni makao makuu ya serikali," alisema.

Kuhusu nyumba za watumishi wa umma zinazojengwa na TBA, alisema mradi huo utakuwa na manufaa makubwa kwani watumishi wataweza kukaa katika nyumba nzuri.

Hata hivyo, aliipongeza TBA kwa kufanya kazi nzuri ikiwamo kuwa na vifaa na wataalamu wa kutosha.

"TBA kwa kweli kwa uwezo niliiouna mimi nadhani hata kama kuna makandarasi wengine kuna miradi mbalimbali ya ujenzi ni kushawishi tu waitumie TBA kama ni mkandarasi waitumie TBA kama ni msimamizi kwa sababu wana uwezo wote wana vifaa wana zana na wana wataalamu wakutosha," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa ZBA, Mhandisi Kassim Omar, alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza yale ambayo TBA wanayafanya ambapo kwa kiwango kikubwa yanalingana na majukumu ya ZBA.

"Zanzibar kwa sasa wapo katika matayarisho ya Mji wa Kiserikali visiwani ambapo utekelezaji wao utakuwa ni mkubwa ambapo amewakaribisha TBA waone yale ambayo wameyaonyesha tutakavyoyatekeleza," alisema Mhandisi Omar.

Naye Kaimu Mkurugenzi Idara ya Miliki TBA, Said Mndeme, alisema ziara hiyo imekuwa na manufaa makubwa kwani ZBA wameweza kuona mradi wa nyumba za watumishi wa umma na wameona jinsi walivyoutekeleza mradi huo na namna ambavyo wamejipanga katika eneo la malighafi pamoja na viwanda mbalimbali ambavyo wamevianzisha.

# Wakimbizi 1,200,000 warejeshwa kwenye nchi zao kwa hiari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema tangu kuanzishwa kwa makambi miaka ya 1990 zaidi ya wakimbizi 1,200,000 wamerejeshwa katika nchi zao za asili kwa hiari.

Aidha, zaidi ya wakimbizi 200,000 wamepewa uraia wa Tanzania wakiwamo Warundi 162,156 wa mwaka 1972 ambao walipewa uraia mwaka 2009/2010.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alibainisha hayo juzi wakati alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya wizara hiyo kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema, wakimbizi wengine ni kutoka Rwanda wapatao 36,000 ambao walipewa uraia miaka ya 1980 na Wasomali 1,430 waliopewa uraia miaka ya 2005 hadi 2010. "Wengine ni wakimbizi kadhaa wanaoishi vijijini waliopewa uraia kwa masharti nafuu miaka ya 1990," alisema Simbachawene.

Aidha, alisema kuwa katika kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi zaidi ya 39,000 wamepelekwa nchi ya tatu katika mpango maalum wakuhamisha wakimbizi nchi ya tatu ulioanza mwaka 2007.

Pia alisema katika kundi la wakimbizi Warundi walioingia nchini kuanzia mwaka 2015, wakimbizi zaidi ya 139,000 wamerejeshwa katika nchi yao ya asili kwa hiari.

"Kwa sasa tunao wakimbizi 255,275 kutoka nchi za Burundi wapo 175,498, Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Kongo wapo 79,337 na mataifa mengine wapo 440," alisema Simbachawene.

Akizungumzia mafanikio ya wizara hiyo katika majeshi yake alisema baada ya uhuru Jeshi la Polisi limejenga nyumba 10,048 za makazi ya maofisa na askari wake katika mikoa mbalimbali nchini.

"Kati ya mwaka 2016 hadi sasa Jeshi la Magereza limejenga nyumba 310 za kisasa zenye uwezo wa kuhudumia familia 564 kwa ajili ya makazi ya maofisa na askari," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa Idara ya Uhamiaji ina jumla ya nyumba 491 za maofisa na askari wake katika mikoa mbalimbali nchini zilizonunuliwa na kujengwa baada ya uhuru.

Kadhalika, alisema Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kujenga nyumba 95 kwa ajili ya makazi ya maofisa na askari katika mikoa mbalimbali nchini ukilinganisha na nyumba za makazi ya askari za kutosha familia 14 zilizokuwapo wakati wa uhuru.





# Elimu stakabadhi ghalani yatakiwa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SERIKALI imewasisitiza maofisa ushirika kutoa elimu ya uuzaji wa mazao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani ili wakulima wa kakao wapate faida.

Wakulima hao wanaolengwa ni wa kakao wilaya za Rungwe, Kyela na Busokelo mkoani Mbeya.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati wa mkutano wa wadau wa zao la kakao ulioshirikisha wakulima wa halmashauri tatu zilizopo mkoani Mbeya ambazo zinajihusisha na kilimo hicho.

"Nasisitiza elimu hii itolewe kwa wakulima wote waliopo katika halmashauri zetu tatu za wilaya za Kyela, Rungwe, pamoja na Halmashauri ya Busokelo...kila mkulima atambue umuhimu wa uuzaji wa mazao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani ili kujipatia faida na kuuza kwa bei wanayoitaka," alisema Homera.

Sambamba na kusisitiza elimu kwa wakulima Homera alisema zao la kakao ni tegemeo kwa wilaya za Kyela na Rungwe kuendesha maisha yao.

Alisema kwamba katika kuboresha mazingira ya zao hilo tayari serikali imeondoa baadhi ya tozo za zao hilo ambazo wakulima walikuwa wanalipa.

Alisema badala ya kulipa shilingi 157 kwa kila gunia sasa atatakiwa kulipa shilingi 33 katika mnada wowote ambao utakuwa ukifanyika katika wilaya za Kyela, Rungwe na Busokelo sawa na punguzo la shilingi 125.

"Mfumo huo utaondoa watu wa kati upigaji na mtandao huo utasaidia usafirishaji au makuli ambao wanawalangua wakulima pasipo kufuata sheria na taratibu," alisema Homera.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Uendeshaji wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Augustino Mbulumi, alisema lengo la taasisi hiyo ni kumwezesha mkulima kuuza kwa ushinani zaidi, na kwamba mnunuzi asilazimishe kununua kakao hadi wakubaliane soko la bidhaa.

Alisema lengo lao ni kumwezesha mkulima kuuza mazao yake kwa ushindani zaidi badala ya kuuza kwa hasara.

"Taasisi yetu imekuwa msaada mkubwa kwa wakulima na tunaendelea kutoa elimu ili mkulima aweze kunufainika na kilimo na asione hasara kuingia kwenye suala la kilimo," alisema.

# PM awahimiza wanaume kupima VVU

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wanaume kujitokeza kupima maambukizi ya Virusi vya Ukimwi ili kujua afya zao badala ya kutegemea majibu ya wake zao wakati wa ujauzito.

Majaliwa aliyasema hayo, wakati akifungua kongamano la kisayansi katika wiki ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani lililofanyika jijini Mbeya.

Alisema mwaka 2018 ulifanyika utafiti ambao ulibainisha kuwa wanaume wengi wanakwepa kwenda kupima maambukizi ya Ukimwi badala yake wanategemea majibu ya wake zao baada ya kupima pindi wanapoenda kujifungua.

Alisema katika kuhakikisha idadi ya wanaume wanaopima, serikali imeweka malengo kwamba ifikapo mwaka 2030 Tanzania isiwe na maambukizi mapya ya Ukimwi, na kwamba wanaume wanapaswa kujua afya zao pamoja na kuanza kutumia dawa kwa usahihi kwa wale wanaogundulika kuwa na maambukizi.

Alisema kuwa mafanikio hayo yanaweza pia kufikiwa hata kabla ya muda huo endapo jamii na wadau wakajitokeza kutoa elimu na kuhamasisha kupima ikiwamo kuuwezesha Mfuko wa kudhibiti Ukimwi kwa kuchangia fedha ili kuepukana na utegemezi.

Alisema hatua iliyofikiwa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) juu ya mapambono ya Ukimwi ni kubwa, lakini inakabiliwa na ukosefu wa fedha, hivyo kila mwananchi anapaswa kuchangia chochote ili mfuko huo uepukane na kutegemea fedha za wafadhili ambazo zina mwisho wake.

"Ili kufikia malengo tuliojiwekea ni lazima tume iwe na fedha zake kupitia mfuko ulioanzishwa kwa wadau na wananchi mmoja mmoja kuchangia fedha kidogo kidogo kwani hadi sasa kazi waliyofanya hawa watu wa Tume ni kubwa sana," alisema Waziri Mkuu.

Aliongeza kuwa njia nyingine ya kufikia malengo hayo ni kuhakikisha hakuna mtoto anayezaliwa akiwa na maambukizi kuanzia sasa ili kuwe na kizazi salama kwa kutoa elimu kwa wanaume pamoja na kinamama kuanzia ngazi ya chini.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Tickson Nzunda, alisema kutakuwa na wadau 150 pamoja na washiriki zaidi ya 500 ambao watajikita katika kujadili namna ya kufanya utafiti, utoaji wa huduma, kuhamasisha jamii, kutoa elimu na kutoa mwelekeo wa namna ya kudhibiti maambukizi mapya ya ugonjwa wa Ukimwi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ukimwi ya Bunge, Fatma Toufiq, alisema kamati itaendelea kuishauri serikali kutenga bajeti ya kutosha ili ifikapo 2030 Tanzania isiwe na maambukizi ya VVU.

Naye Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboki, alisema kongamano hilo ni la sita kufanyika tangu kuanzishwa ambalo hufanyika kila wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, ambapo wadau huja na mapendekezo na maoni yanayopaswa kufanyika.

Aliongeza kuwa katika kongamano hilo jumla ya mada 34 zitajadiliwa kwa mdomo kati ya mada 57 zilizopo, na kwamba zinazobaki zitawasilishwa kupitia mabango mbalimbali yatakayowekwa ukumbini.

Naibu Waziri wa Afya, Godwin Mollel, alisema katika mapambano dhidi ya Ukimwi serikali imetenga shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya wanasayansi kufanya utafiti wa sayansi tiba ili baadaye wajikite kwenye uzalishaji.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Kituo cha Songwe, Godlove Longole (kulia), akifafanua namna ambavyo serikali inashiriki kwenye shughuli za kijamii kutokana na uwepo wa Rada Reno ya Lumbila mkoani Songwe, kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mkumba, wakati wa ziara mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Miundombinu ya rada yatengewa mamilioni

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imetumia shilingi milioni 67 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya rada iliyojengwa katika Kijiji cha Iyula, Wilaya ya Mbozi mkoani.

Lengo ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa usalama wa anga kupitia ndege za ndani na nje ya nchi. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Kituo cha Songwe, Godlove Longole, ameyasema hayo wakati wa ziara iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, kukagua shughuli mbalimbali zinazofanyika katika rada hiyo kuanzia Uwanja wa Ndege wa Songwe hadi ilipojengwa rada eneo la Lumbila.

Alisema rada ya Lumbila ndio pekee ambayo imejengwa nje ya uwanja na kwenye miinuko kutoa taarifa mbalimbali za hali ya ndege na abiria wawapo safarini.

Longole alisema Tanzania ina rada nne ambazo mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Songwe na Kilimanjaro, na kwamba zote zinafanya kazi ya kupata taarifa mbalimbali za kiusalama na hali ya usafiri wa ndege za kitaifa na kimataifa.

"Ziara hii ina lengo la kuwapa nafasi viongozi wa serikali kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na rada zetu, watajua namna zinavyofanya kazi kwa ajili ya kulinda usalama wa nchi na mataifa jirani kupitia usafiri wa anga na namna wananchi wanaweza kutunza miundombinu ili kazi zifanyike bila changamoto," alisema Longole.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wananchi wanaozunguka eneo la rada hiyo wananufaika, serikali inaendelea kuunga mkono jitihada mbalimbali wanazozifanya ambapo hadi sasa wamechangia shilingi milioni nane kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Kwa upande wake, RC Mgumba aliishukuru serikali kwa ujenzi wa rada hiyo, na kwamba wamejipanga kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi kupitia anga la Uwanja wa Ndege wa Songwe.

Alisema katika kufanikisha hilo, wametenga zaidi ya ekatri 900 kwa ajili ya kilimo cha mboga na matunda ili kuuza na kusafirisha bidhaa hizo kwa kutumia Uwanja wa Songwe.

Baadhi ya wakazi wa Lumbila Kata ya Ruanda mkoani Songwe walisema uwapo wa rada hiyo umefungua fursa mbalimbali za kiuchumi.





# Kasi yatakiwa hukumu kesi za udhalilishaji wa kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAIMU Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdallah, amewataka mahakimu na majaji wanaoendesha kesi za udhalilishaji wa kijinsia kuharakisha zinatolewa hukumu haraka.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya haki za binadamu kwa mawakili na majaji wa mahakama za Zanzibar yaliyofanyika Mjini Zanzibar, ambayo yameandaliwa na Taasisi ya Utetezi wa Haki za Binadamu Tanzania.

Alisema serikali imeongeza mahakimu 10 wa Mahakama Maalum ya Udhalilishaji ili kuharakisha usikilizaji wa kesi hizo, hivyo ni vyema kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi, hali ambayo itapunguza malalamiko ya wanajamii kuhusu kuchelewa kutolewa hukumu kwa kesi hizo.

Alisema kuna makosa mengi ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto yaliyofikishwa mahakamani, hivyo mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa kuzidisha kasi ya usikilizaji wa kesi hizo na kutoa uamuzi wa haraka.

Alisema hivi sasa mahakama imepunguza muda wa usikilizaji wa kesi za udhalilishaji ambapo awali kesi hizo zilikuwa zinachukua muda wa miaka mitatu hadi kutolewa hukumu, lakini kwa sasa ni muda wa mwaka mmoja tu.

Alitoa wito kwa majaji na mahakimu kushughulikia kesi bila ya woga au upendeleo na kuhakikisha wanafuata sheria.

Alisema jamii imekuwa ikiwalalamikia majaji na kuwahusisha na vitendo vya rushwa na ucheweleshaji wa kesi, hivyo aliwasisitiza kuachana na mambo hayo ambayo ni kinyume cha sheria ili kujenga imani kwa wananchi.

"Maamuzi ya mahakama hayatolewi na mahakama pekee bali ni kushirikiana na wadau wengine wa mahakama, hivyo niwasihi wadau hao ikiwamo wananchi kuwa na ushirikiano na mahakama na pale wanapohitajika kufika mahakamani kutoa ushahidi wasisite, wafikike mahakamani," alisema.

Aidha, alisema upatikanaji wa nakala za hukumu mahakamani wameliundia kamati ili kupatikana kwa haraka kwa sababu haki inapocheleweshwa ni haki inayozuiwa.

Jaji huyo alisema serikali imejipanga kuleta mabadiliko makubwa katika utendaji wa mahakama, na itahakikisha inapopandisha madaraja kwa mahakimu wataangalia usikilizaji wa kesi kwa kila hakimu ambae atakuwa amesikiliza kesi nyingi za kuzitolea hukumu kwa haraka ndiye atakayepewa nafasi hiyo ya kupandishwa daraja.

Naye Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Onesmo Olengurumwa, alisema kuwa mafunzo hayo yanalenga kuwakumbusha misingi ya haki za binadamu kwa majaji na mahakimu.

Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Salma Ali Hassan, alisema kuwa mfungwa ana haki zake anazostahiki kuzipata ikiwamo haki ya faragha na kupata haja kubwa au ndogo katika hali ya staha.

## SMZ yajipanga kuboresha Afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kuimarisha sekta ya afya hususan katika uimarishaji wa miundombinu na kubainisha kutumia kikamilifu mkopo iliyopata kutokana na fedha za UVIKO-19.

Hayo yalielezwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ikulu Zanzibar wakati akizungumza na uongozi wa Bodi ya Taasisi ya 'Mkapa Foundation', iliongozwa na Mwenyekiti wake Dk. Adeline Kimambo.

Dk. Mwinyi alipongeza juhudi zinazochukuliwa na Taasisi ya 'Mkapa Foundation' katika kuimarisha sekta ya afya na kusema kwamba inathamini michango mbalimbali inayotolewa na taasisi hiyo, ikiwemo upatikanaji wa ajira kwa watumishi wake.

Alisema kuwa serikali inakusudia kutengeneza utaratibu utakaowezesha watumishi walioajiriwa na taasisi hiyo kuingia katika mfumo wa serikali baada ya muda wa utumishi wao kumalizika kulingana na mikataba yao.

Dk. Mwinyi ameishukuru Bodi ya Taasisi ya 'Mkapa Foundation' kwa kuona umuhimu wa kuichagua Zanzibar kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka miwili ya kifo cha Hayati Benjamin Mkapa mwaka 2022.

Aidha, aliishukuru taasisi hiyo kwa kazi kubwa inayofanya, na kusema kwamba serikali itashirikiana nayo ili kufanikisha maadhimisho hayo yanayotarajiwa kufanyika mwezi Julai 2022, sambamba na kuahidi kuchangia mfuko wa Wakfu wa Taasisi hiyo.

Naye Mtendaji Mkuu wa Bodi ya 'Mkapa Foundation', Dk. Ellen Mkondya Senkoro, alisema maadhimisho ya kumuenzi Hayati Rais Benjamin Mkapa mwaka 2022 yatafanyika Zanzibar, ambapo yataambatana na shughuli mbalimbali ikiwamo kongamano pamoja na hotuba za kitaifa.

Alisema bodi hiyo iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya maadhimisho hayo, ikijipanga kutuma maombi kwa Serikali ya Zanzibar ili kupata wajumbe watakaoingia katika kamati ya maandalizi.

Mtendaji huyo alisema kuanzia Oktoba mwaka 2021, Taasisi ya 'Mkapa Foundation' imeanza utekelezaji wa programu mbalimbali Zanzibar, ikiwamo ya kupambana na magonjwa ya UVIKO-19 na kifua kikuu.

Alisema taasisi imeajiri wafanyakazi wa kada mbalimbali katika sekta ya afya wapatao 105 Unguja na Pemba ambao wamesambazwa katika vituo 33 vya utoaji huduma, bandarini na viwanja vya ndege, ambapo miongoni mwao watafanyakazi kwa mikataba ya miezi tisa na watumishi watano kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Aidha, alisema taasisi hiyo imeendesha mafunzo mbalimbali kwa watendaji hao ikiwamo ya maadili ya utumishi wa umma, mama na mtoto na COVID -19, huku matokeo ya awali yakionyesha kuwapo mafanikio ya ongezeko la wananchi wanajitokeza kupata chanjo kuchanja ya corona.




Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman, akizungumza na Jumuiya ya Mawakili wa Afrika Mashariki, kuwapongeza kwa jitihada wanazozichukua kushajihisha utawala wa sheria, katika mkutano uliofanyika, mjini hapa, alimwakilisha Rais Dk. Mwinyi. **PICHA: RAHMA SULEAIMAN**

# Mwinyi avipongeza vyama vya mawakili EA kushirikiana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amevipongeza vyama vya mawakili kutoka Afrika Mashariki kwa jitihada zao za kufanya kazi pamoja, jambo ambalo linasaidia kukuza uwelewa wa masuala ya kisheria katika nchi wanachama.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alieleza hayo kwa niaba ya Rais Dk. Mwinyi katika mkutano wa 26 wa vyama vya mawakili vya Afrika Mashariki uliofanyika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema umoja huo unasaidia kupaza sauti zao sambamba na kubadilishana uzoefu kupitia mafunzo mbalimbali yanayotolewa katika mikutano hiyo.

Alieleza kuwa kupitia mikutano hiyo ya vyama vya mawakili mbali na kusaidia kupaza sauti zao, lakini inasaidia kushajihisha utawala wa sheria na kuruhusu kubadilishana uzoefu kupitia nchi zilizomo katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Kupitia mkutano huo, Hemed aliuhakikishia umoja wa vyama vya mawakili kuwa Serikali ya Zanzibar inaunga mkono na kuthamini jitihada zinazochukuliwa na wanachama wa umoja huo pamoja na kutambuliwa na uongozi wa ngazi mbalimbali za serikali zilizomo ndani ya nchi za Afrika Mashariki.

Alifafanua kwamba, kwa vile jukumu la kushajihisha utawala wa sheria haliishii mikononi mwa wanasheria pekee, Serikali ya Zanzibar imechukua jitihada za makusudi katika kushajihisha suala ilo kupitia Katiba ya Zanzibar kifungu namba 5 cha Katiba ya Zanzibar.

"Zanzibar itakuwa nchi yenye kufuata mfumo wa vyama vingi ambao utazingatia mfumo wa utawala wa sheria, haki za binadamu, amani, haki na usawa," alieleza Hemed kwa niaba ya Dk. Mwinyi.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haruna Ali Suleiman, alisema serikali itaendelea kushirikiana na viongozi wa Chama cha Mawakili Zanzibar katika kuzitatua changamoto zilizokuwapo. Rais wa Vyama vya Mawakili Afrika Mashariki, Bernard Oundo, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa hatua waliofikia katika kustawisha utala bora kwa kuanzisha wizira maalum inayohusiana na masuala ya sheria, katiba na utawala bora, jambo ambalo ndio msingi wa ukuzaji wa uchumi wa Nchi katika nyanja zote.

Alisema kuna kila sababu ya kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuja na sera ya dhana ya uchumi wa bluu na kuahidi kuwa kupitia umoja huo utaunga mkono sera hiyo kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi na maendeleo ya watu wake. Rais wa Chama cha Mawaiili Zanzibar, Slim Abdulla, alisema kufanyika kwa mkutano huo kutasaidia kwa wanasheria wa ndani kujitathmini kupitia huduma za kisheria wanazozitoa ili kujiridhisha kama zinakidhi matakwa ya kikanda.

# Waziri: Ujenzi lazima uzingatie mipango miji

**Na Munir Shemweta, SHINYANGA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekagua ujenzi wa nyumba katika Manispaa ya Shinyanga kuona kama unafanyika kwa kufuata taratibu za mipango miji pamoja na maelekezo ya kitaalamu.

Akiwa katika ziara yake ya siku mbili mkoani Shinyanga mwishoni mwa wiki Dk. Mabula alibaini kukiukwa kwa baadhi ya taratibu na watu wanaofanya ujenzi kwenye eneo jipya la Mwalugoye katika Manispaa ya Shinyanga.

Baadhi ya taratibu zilizokiukwa ni nyumba za makazi kuwekwa maduka ya biashara, kujengwa kiwanda cha kufyatulia tofali eneo la makazi pamoja na baadhi ya nyumba kuezekwa bila kufuata ushauri wa kitaalamu.

Mabula ambaye aliambatana na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Yasinta Mboneko, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na timu ya wataalamu wa sekta ya ardhi, alishangazwa na namna ujenzi unavyoendelea kwa kasi huku kukiwa hakuna ufuatiliaji wa kujua kama wanaojenga wanafuata taratibu.

"Maeneo mapya mkiyaacha tu watu watajenga bila kufuata taratibu, tunahitaji kule tunapopanga na kuendeleza taratibu za mipango miji zisimamiwe ili tuone tofauti ile miji iliyojengwa zamani na hii ya sasa na msipofuatilia watu wanajua business as usual," alisema Mabula.

Aliitaka Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kuhakikisha inasimamia sheria na taratibu ili wote wanaofanya ujenzi katika eneo hilo wazingatie taratibu za mipango miji na wanaojenga bila vibali wanasimamishiwa ujenzi.

"Hili ni eneo jipya, lakini watu wanaendelea kujenga bila kuzingatia taratibu, simamieni taratibu na sheria na mhakikishe wote wanaojenga wana vibali vya ujenzi na mtu asiye na kibali simamisheni ujenzi mapema msisubiri mpaka afike kwenye linta ndiyo mmwambie abomoe huko ni kumwonea," alisema Dk. Mabula.

Aliwataka watendaji wa mitaa kuwasaidia Wakurugenzi wa Halmashauri nchini kwa kuhakikisha wanaofanya ujenzi wanakuwa na vibali ili maeneo yaliyopangwa yasivurugwe. Alisisitiza kuwa, wasiposimamia vizuri maeneo yao basi watakuta maeneo yaliyopangwa yamevurugwa na kuifanya miji kutokuwa salama.

Pia alizitaka halmashauri kupitia watendaji wa ardhi kuwakumbusha wamiliki wa ardhi walioshindwa kuendeleza maeneo yao kuyaendeleza kwa mujibu wa sheria na watakaoshindwa basi maeneo yao wapatiwe watu wengine wenye uhitaji na kusisitiza kuwa sheria lazima isimamiwe sambamba na kuwahimiza wamiliki kulipa kodi ya pango la ardhi.

# Museveni kumkabidhi Rais Samia shule wilayani Chato

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajia kumpokea Rais wa Uganda, Yoweri Museveni leo wilayani Chato, atakayekuwa kwenye ziara ya siku moja nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, alisema lengo la ziara hiyo ni makabidhiano ya Shule ya Msingi Museveni iliyopo katika Kijiji cha Nyabilezi, Wilaya ya Chato.

Senyamule alisema shule hiyo imejengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Uganda chini ya Rais Museveni na ndiye anayetarajiwa kumkabidhi Rais Samia shule hiyo ambayo ujenzi wake ulianza Februari 11, 2020 na kukamilika Februari 11, 2021.

Aidha, alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ya msingi 17, madarasa ya awali matatu, jengo la utawala moja, matundu ya vyoo 37, ofisi mbili, maktaba moja na nyumba za walimu. Ujenzi huo umekamilika kwa asilimia 100.




Mkurugenzi wa huduma za kidigitali wa Vodacom Tanzania, Nguvu Kamando, akiwahutubia washiriki wa mkutano wa 20 wa taasisi za kifedha uliokuwa ukijadili uchumi wa Tanzania baada ya janga la COVID-19. Mkutano huo ulifanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi waja kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi

**NAIROBI, KENYA**

KATIKA juhudi za kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kampuni ya Qnet imezindua mradi wa upandaji miti uitwao 'Urithi wa Kijani', unaolenga kuhamasisha upandaji na utunzaji wa miti barani Afrika.

Kupitia mradi huu, shirika hilo limepanda zaidi ya miti 3,000 barani Afrika na Asia. Kenya, mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya vijijini chini ya ushirikiano na kikundi kiitwacho Trees4Kenya.

"Kwa kushirikiana na Trees4Kenya, tunajitahidi kubadilisha kiwango cha kaboni cha Kenya na tuna nia ya kujenga jumuiya endelevu kote barani Afrika," alisema Mratibu wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Qnet, Muqtadir Suwani.

Suwani alikuwa akizungumza hivi majuzi nchini Kenya wakati wawakilishi wa kampuni hiyo walipotembelea maeneo ya upandaji miti huko Embu, Kenya.

"Hakuna wakati kama wa sasa wa kuwa rafiki na mazingira...Qnet inaunga mkono jitihada za serikali kutunza mazingira na kuleta mabadiliko chanya," aliongeza.

Suwani aliendelea kuelezea mradi huo kama ushirikiano wa wadau mbalimbali unaofanya kazi katika ngazi ya jamii kupitia ushirikiano na wadau kama vile EcoMatcher na kikundi cha Trees4Kenya.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Trees4Kenya, Paulino Mugendi, alisema ushirikiano huo wa sekta binafsi ni muhimu ili kuokoa misitu ya Kenya.

"Tunashukuru sana Qnet na washirika wao kwa msaada huu...ni kwa kupanda miti tu ndipo tunaweza kulinda mazingira yetu vyema," alisema mwanamazingira huyo.

"Tayari tumepanda mamia ya miti na kupitia mradi huu tunatarajia kupanda zaidi ya miti 1000 na kwa njia hiyo kusaidia kurejesha misitu nchini Kenya," aliongeza.

Pia alikuwapo Karuku Kathogo, mtaalamu wa misitu kutoka Forestry Kenya ambaye alisema zaidi ya kulinda mazingira, kupanda miti pia kunasaidia maendeleo endelevu ya jamii.

"Mipango hii inahakikisha kwamba tunakuwa na jumuiya endelevu ambayo haiharibu mazingira yake kwa jina la maendeleo," alisema.

Marehemu Wangari Mathai, mwanzilishi wa Green Belt Movement nchini Kenya aliwahi kusema, "...watu maskini watakata mti wa mwisho ili kupika mlo wa mwisho."

Mwanamazingira alisema maneno hayo akimaanisha jitihada za utunzaji mazingira lazima ziende ana kwa ana na utokomezaji wa umaskini. Mathai alihamasisha upandaji wa zaidi ya miti milioni 30, na kuhamasisha Umoja wa Mataifa kuanzisha kampeni ambayo imesababisha kupanda miti bilioni 11 duniani kote.

Hata hivyo, kwa vile umaskini unazidi kushamiri, Afrika sasa inapoteza misitu mingi kila siku na jambo la kusikitisha ambalo lilifichuliwa katika mkutano wa COP26 mwaka huu ni kwamba Afrika bado haipewi ufadhili unaohitajika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

# Taliban yasisitiza elimu kwa wote

**Kabul, AFGHANISTAN**

KAIMU Waziri Mkuu wa serikali ya mpito ya Taliban, amesema katika hotuba yake kuwa elimu kwa wasichana pamoja na wavulana ni lazima, akiashiria kuwa wasichana wataruhusiwa kwenda shule kama hali itaruhusu.

Mullah Hasan Akhund, aligusia kuhusu suala la wasichana kutoruhusiwa kurejea tena kwenye elimu ya sekondari kwenye mji mkuu wa nchi hiyo Kabul na kwingineko.

Shirika la habari la taifa la Afghanistan, lilitangaza sauti ya hotuba yake, mwishoni mwa wiki.

Alisema elimu ni lazima kwa wavulana na wasichana wa Kiislamu.

Aliashiria kuwa pale shule zitakapokuwa tayari kuratibu elimu tofauti kwa watoto hao, wasichana wataanza kwenda shuleni hatua kwa hatua.

Akhund, alisema wanawake Afghanistan wapo huru kwenda mahala popote na kujipatia elimu na kufanya kazi. Aliongeza kwamba, wanafurahia amani.

**NHK**

# Wanajeshi Sudan wauawa katika shambulizi

**Khartoum, SUDAN**

WANAJESHI sita wa Sudan, wameuawa katika shambulio lililofanywa na wanajeshi wa Ethiopia dhidi ya kituo cha jeshi la Sudan, karibu na mpaka kati ya nchi hizo mbili.

Jeshi la Sudan, limeliarifu shirika la habari la Uingereza la Reuters.

Awali pasipo kutoa ufafanuzi zaidi katika taarifa kupitia mtandao wa Facebook, jeshi hilo la Sudan lilisema kuwa makundi ya wanajeshi na wanamgambo yalishambulia wanajeshi wake katika eneo la Al- Fashaga Al-sughra na kusababisha vifo.

Shirika la habari la Reuters, halikumpata msemaji wa serikali ya Ethiopia, Legesse Tulu, ili kuzungumzia mara moja juu ya mkasa huo.

**DW**

**Awali pasipo kutoa ufafanuzi zaidi katika taarifa kupitia mtandao wa Facebook, jeshi hilo la Sudan lilisema kuwa makundi ya wanajeshi na wanamgambo yalishambulia wanajeshi wake katika eneo la Al- Fashaga Al-sughra na kusababisha vifo.**

# Kenya yajizatiti na kirusi Omicron

**Nairobi, KENYA**

KENYA imepiga marufuku kusafiri kwenda Kusini mwa Afrika, pia Wizara ya Afya inasema, itawachunguza kwa makini watu wanaowasili kutoka Afrika Kusini, Botswana na Hong Kong kubaini kama wana virusi vipya vya Covid-19, vilivyogunduliwa nchini Afrika Kusini.

Serikali ya Kenya imewaelekeza abiria wanaowasili kutoka nchi za Kusini mwa Afrika, kupima Covid-19, kabla ya kuruhusiwa kuingia nchini humo.

Afrika Kusini na Botswana, zimeripoti virusi vipya katika nchi zao, wanasayansi walisema vinaambukiza kwa kasi kubwa na ni sugu kwa chanjo.

Mkurugenzi Mkuu wa Afya Kenya, Patrick Amoth, aliiambia shirika la habari la Marekani VOA, kwamba nchi yake iko katika hali ya tahadhari kubwa, kupambana na virusi vipya.

"Tunafanya kazi kuhakikisha kwamba mfumo wetu wa ufuatiliaji ni wa hali ya juu na kuwaangalia haswa watu wanaokuja kutoka Afrika Kusini, Botswana na Hong Kong ili kuwaingiza katika mfumo imara wa ufuatiliaji.

"Tunasisitiza wawe wamepokea chanjo kamili kabla ya kuja nchini. Pia unatakiwa kuwa na majibu ya PCR kwamba huna virusi ambayo yametolewa ndani ya muda wa saa 96 kabla ya kuwasili nchini," Amoth alisema.

Wiki hii Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alisafiri kwenda Afrika Kusini, ambako alitia saini makubaliano ya kuboresha biashara na ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi hizo mbili.

Ili kupambana na kusambaa kwa virusi kwa watu, Kenya imezindua kampeni kabambe ya siku 10 kuanza Ijumaa wiki iliyopita na imefanikiwa kuwapatia chanjo takriban watu milioni 6.5.

Amoth alisema wana chanjo za kutosha kuwapatia watu wengi zaidi.

"Ni sehemu ya mchakato wa chanjo unaoendelea na tunataka kuzidisha hali kulingana na matukio ambayo yanatokea huko Ulaya na kwingineko duniani.

"Kwa hiyo ili kuhakikisha tunafikia watu wengi zaidi waliopata chanjo kwa lengo la kuwalinda watu nchini na hivi sasa tuna chanjo za kutosha kuongeza idadi ya watu kupatiwa chanjo," aliongezea Amoth.

Amoth alielezea imani yake kwamba Wakenya wengi zaidi watapatiwa chanjo.

Kenya, ina sera ya kutotoa huduma za serikali kwa watu ambao hawakupatiwa pia wanawashawishi watu kujitokeza kupatiwa chanjo.

Inatarajia kuwapatia chanjo watu milioni 10 ifikapo mwisho wa mwaka huu.




Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Tshwane wakirejea kwenye makazi yao mjini Pretoria, Afrika Kusini, mwishoni mwa wiki. Jumamosi, imetangazwa hali ya tahadhari baada ya kirusi kipya cha Omicron cha corona kubainika. **PICHA: AP**

# Afrika Kusini yasema Omicron sio hatari

**Johannesburg, AFRIKA KUSINI**

CHAMA cha Madaktari Afrika Kusini (SAMA), kimesema watu ambao wamepata maambukizo ya aina mpya ya virusi vya Covid-19 ya Omicron, hawajaugua kwa kiwango kikubwa.

Mwenyekiti wa chama hicho, Angelique Coetzee, aliliambia shirika la utangazaji la BBC, akisema kwa wakati huu visa vilivyogunduliwa havijafika katika kiwango kibaya.

Alisema idadi kubwa ya wagonjwa wanalalamikia maumivu ya mwili na uchovu mkali na kwamba wanaowashuhudia kwa sasa ni vijana zaidi na si watu wazima.

Hata hivyo, alisema utafiti kuhusu aina hiyo mpya ya virusi bado upo katika hatua ya mwanzo na kuongeza pia takwimu za taifa hilo zinaonyesha asilimia 24 tu ya raia ndio waliokamilisha chanjo.

Taasisi ya Kudhibiti Magonjwa barani Ulaya, imeonyesha wasiwasi mkubwa kuhusu aina hiyo mpya ya virusi, kwamba inaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa uwezo wa chanjo zilizopo na kutoa nafasi ya watu kuambukizwa tena.

**DW**

# TEMBO WARRIORS YAANZA VEMA, KARAFU YAPIGWA DAZENI CANAF

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Timu ya Taifa ya Tanzania Bara ya Wenye Ulemavu, Tembo Warriors ilianza vema michuano hiyo ya Afrika (CANAF 2021) kwa kuifunga Morocco mabao 2-1, ndugu zao wa Zanzibar 'Karafu Empire', jana ilipokea kipigo cha mabao 12-0 kutoka kwa timu ya Taifa ya Angola.

Hadi mapumziko, tayari Zanzibar ilikuwa imeshafungwa idadi hiyo ya mabao, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Mashindano hayo ya Afrika ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu, ambayo yalianza kutimua vumbi Novemba 27, mwaka huu hapa nchini na kufunguliwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, timu nane zitakazotinga robo fainali zitafuzu moja kwa moja Kombe la Dunia mwakani nchini Uturuki.

Karafu Empire ambayo imepangwa Kundi B pamoja Kenya, Rwandana na Angola ambayo ambayo ni nchi ya kwanza Afrika kuchukua Kombe la Dunia kwa Walemavu.

Nchi nyingine zilizowahi kubeba ubingwa huo ni Urusi ambayo iliubeba mara nne mwaka 1998, 2002, 2003 na 2014 huku Brazil ikiutwaa mara tatu mwaka 2000, 2001 na 2005 kama ilivyo kwa Jamhuri ya Uzbekistan, mwaka 2007, 2010 na 2012.

Tembo Warriors ipo Kundi A pamoja na nchi za Sierra Lionne, Uganda na Morocco, wakati Kundi B likiundwa na Angola, Kenya, Rwanda na Zanzibar, Kundi C ipo Liberia, Cameroon, Gambia na Ethiopia na Kundi D ni Nigeria, Ghana na Misri.

TUPO TAYARI...




Wachezaji wa Yanga, wakiwasili Uwanja wa Ndege wa Mbeya, tayari kwa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Mbeya Kwanza itakayopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine kesho. **PICHA: YANGA**

# Jeremiah afungua pazia hat-trick Ligi Kuu 2021

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Prisons imeshinda mechi ya kwanza kwenye Ligi Kuu baada ya kushuka dimbani mara sita msimu huu bila ushindi, huku straika wake Jeremiah Juma akiwa mchezaji wa kwanza msimu huu kufunga mabao matatu kwenye mechi moja, 'hat-trick'.

Kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Sumbawanga juzi, maafande hao wa Magereza, walitoa kipigo cha kushtukiza cha mabao 3-1 dhidi ya Namungo, ukiwa ni mchezo wa kwanza kwao tangu kuanza kwa Ligi Kuu msimu huu.

Mchezaji aliyeionjesha tamu ya ushindi kwa mara ya kwanza, Jeremiah, ameweka rekodi kuwa mchezaji wa kwanza kupiga 'hat-trick' msimu huu.

Jeremiah alifunga dakika ya tatu, 10 na 26, huku bao la kufutia machozi la Namungo likifungwa na Mnyarwanda Bigirimana Blaise, baada ya kupokea pasi kutoka kwa Mzambia Obrey Chirwa.

Jeremiah amefunga 'hat-trick' kwenye raundi ya saba, na kuvunja rekodi ya msimu uliopita ilipopatikana kwenye raundi ya nane.

Mchezaji aliyekuwa wa kwanza kufunga 'hat-trick' msimu uliopita ni Adam Adam wakati huo akiichezea JKT Tanzania akifunga dakika ya 23, 48 na 83, kwenye raundi ya nane, timu yake ikiizabua Mwadui FC mabao 6-1 kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, Shinyanga. Kwa sasa mchezaji huyo anaichezea Polisi Tanzania.

Ni ushindi ambao umeipeleka Prisons hadi kwenye nafasi ya nane kwa pointi nane kabla ya mechi za jana jioni na usiku, ikicheza mechi saba hadi sasa.

# Kocha KMC sasa kufungia kazi beki

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa KMC FC, Habib Kondo, amesema anakwenda kuifanyia kazi safu yake ya ulinzi, baada ya kuruhusu mabao mawili juzi dhidi ya Mbeya City na kusababisha sare ya mabao 2-2.

KMC ililazimika kurejesha mabao mara mbili baada ya kutanguliwa na kufanya mechi hiyo kwenda sare, ikiwa ni mechi ya raundi ya saba ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliochezwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

**"Lilikuwa ni pambano zuri, wapinzani wetu walikuwa wanacheza mipira mirefu ambayo kwa wakati fulani ilikuwa ikitutatiza. Tulikuwa na matatizo kwenye safu ya ul inzi, lakini hili tunak wenda kulifanyia kazi, ingawa nimeridhika na pointi moja ya ugenini ambayo ni meipata," alisema Habib, mchezaji wa zamani wa Sigara, Pan African na Reli ya Morogoro.**

Naye mchezaji Mateo Antony mmoja wa wafungaji wa mabao hayo alisema amefurahi kuwa mmoja wa wafungaji kwenye mechi hiyo ambayo alidai kuwa ilikuwa ngumu na hawakutaka kupoteza.

Mchezaji huyo wa zamani wa Yanga, alisema wapinzani wao walitumia zaidi mipira mirefu, huku wao wakicheza kwa pasi fupi fupi, lakini kila timu ilifanya makosa na wenzao wakayatumia.

Kwa matokeo hayo, KMC inafikisha pointi sita kwa mechi saba ilizocheza, ikiwa kwenye nafasi ya 14 kabla ya mechi za jana, huku Mbeya City ikifikisha pointi 11 kwa mechi saba ilizocheza, ikiwa imekwea hadi nafasi ya tatu, kabla ya mechi zingine za Ligi Kuu zilizochezwa jana jioni na usiku.

## ZISIKUPITE

### UNITED WAMTUMAINI HAALAND
MANCHESTER United wanaamini kuwasili kwa Ralf Rangnick pale Old Trafford kutawapa faida katika kinyang'anyiro cha kumsajili Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21 kutoka Borussia Dortmund majira yajayo ya joto. **(Mirror)**

### TARKOWSKI HUYO WEST HAM
KOCHA wa West Ham, David Moyes, anajiandaa na karata yake ya mwisho kumsajili mlinzi wa Burnley, James Tarkowski huku nyota huyo akitarajiwa kuwa mchezaji huru**. (Sun)**

### VLAHOVIC APANGIWA BEI
KLABU ya Fiorentina imewekewa bei ya pauni milioni 55 ya kumuuza mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic ili kuzuia nia ya Manchester United, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, hatarajiwi kuhama Januari. **(Mail)**

### LACAZETTE NA HATIMA YAKE
NYOTA wa Arsenal, Alexandre Lacazette, amesema mawakala wake wanafikiria wapi atakwenda huku mkataba wa mshambuliaji huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 30, ukitarajiwa kukamilika msimu wa majira ya joto. **(Telefoot via Athletic)**

### POGBA KUTOSAJILIWA MADRID
REAL Madrid hawatamsajili kiungo wa kati wa Manchester United, Paul Pogba msimu ujao wa majira ya joto ingawa klabu hiyo imekuwa ikihusishwa kwa kiasi kikubwa na mpango wa kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. **(Marca)**

### PSG KUTOMWACHIA POCHETTINO
KLABU ya Paris St-Germain haina mpango wa kumwachia Mauricio Pochettino kwenda Manchester United katikati ya msimu huu, lakini wako tayari kwa mazungumzo mwishoni mwa msimu. **(Goal)**

### COUNTINHO KWENDA NEWCASTLE
KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 29, anaweza kuhamia Newcastle katika dirisha la uhamisho la Januari - ingawa Mbrazili huyo alikataa kuhamia klabu hiyo ya Ligi Kuu. **(El Nacional)**

### GUARDIOLA HATAKI TIMU EPL
PEP Guardiola amesema Manchester City itakuwa klabu pekee ya England atakayoinoa, kwani hana mpango na kujiunga na timu yoyote kwenye ligi hiyo atakapoondoka pale Etihad. **(Manchester Evening News)**

### FEKIRD KUONGEZA MKATABA
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Nabil Fekir mwenye umri wa miaka 28, yuko mbioni kufanya makubaliano na Real Betis kuhusu mkataba mpya. **(Mundo Deportivo)**

### PALACE WAMTAKA MAYORAL
CRYSTAL Palace wanamfuatilia mshambuliaji wa Hispania, Borja Mayoral, huku mchezaji huyo mwenye miaka 24 akipambana kupata nafasi ya kucheza akiwa kwa mkopo AS Roma akitokea Real Madrid. **(Sun)**

### WAWILI KUTUA ASTON VILLA
MTENDAJI Mkuu wa Aston Villa, Christian Purslow, amesema kunaweza kuwa na mchezaji "mmoja au wawili" watakaoingia Villa Park wakati wa dirisha la usajili la Januari. **(Birmingham Mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AANIKA SIRI YA USHINDI ARSENAL

Neno lilikuwa utulivu, unatakiwa kushinda mara zote, kwa ujumla nimeridhishwa na matokeo pamoja na...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amewasifia wachezaji wa Arsenal kwa utulivu wao kwenye mchezo dhidi ya Newcastle United baada ya kutokuwa kwenye "kiwango bora" katika kipindi cha kwanza wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0, juzi Jumamosi.

'Washikabunduki' hao walianza kufunga kwa bao la Bukayo Saka kabla ya Gabriel Martinelli kufunga la pili sekunde ya 93 baada ya kuingia uwanjani.

Kipigo hicho kiliifanya Newcastle kutoshinda mchezo wowote katika mechi 13 za ufunguzi za Ligi Kuu kwa msimu huu.

Arteta aliridhishwa na kiwango cha timu yake kilichotoka kuchezea kipigo cha mabao 4-0 dhidi ya Liverpool wiki iliyopita.

"Nina furaha na pointi tulizopata baada ya kutoka kupoteza (kwa Liverpool)," alisema Arteta akiiambia BT Sport baada ya mchezo huo.

"Unatakiwa kushinda mara zote. Kwa ujumla nimeridhishwa na matokeo pamoja na kiwango.

"Neno lilikuwa ni kuwa watulivu. Hatukuwa na mchezo mzuri kipindi cha kwanza na ndio maana tukafanya hivyo kipindi cha pili. Tulipata nafasi na tukafunga."

Arsenal walipiga mashuti 12 kipindi cha kwanza na yalikuwa mengi zaidi msimu huu wakizidiwa na Manchester United waliopiga mashuti 15 dhidi ya Aston Villa katika kipindi cha kwanza.









# HAALAND AWEKA REKODI MPYA BUNDESLIGA

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland alihitaji dakika saba kufunga akitoka kuuguza majeraha yake na kufikisha bao la 50 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, juzi Jumamosi.

Kabla ya kurudi uwanjani, Halaand, alikuwa nje ya dimba tangu Oktoba kutokana na maumivu ya misuli.

Halaand alifunga bao hilo akitokea benchi na kuweka rekodi mpya ya kuwa mchezaji kijana zaidi kufikia mabao hayo kwenye ligi hiyo, wakati Borussia Dortmund ikitoka nyuma na kuifumua Wolfsburg 3-1.

Nyota huyo wa kimataifa wa Norway amefikisha idadi ya mabao 50 akiwa na umri wa miaka 21 na siku 129, na kumfanya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufikisha idadi hiyo kwenye historia ya Bundesliga.

Wout Weghorst alianza kuwapa Wolfsburg bao la uongozi kabla ya penalti ya Emre Can na Donyell Malen kupindua matokeo na Haaland kufunga la tatu.

Dortmund ilipaa kileleni mwa msimamo kwa muda, lakini Bayern Munich iliwachapa Arminia Bielefeld bao 1-0 na kurudi kileleni.

Bao hilo pekee lilifungwa na Leroy Sane kwa shuti kali nje ya boksi la penalti.

Bayern Munich sasa imefikisha mabao 102 kwenye Bundesliga kwa mwaka 2021, wakiivunja ile ya Cologne ya kufunga mabao 101 mwaka 1977.

Bao hilo la Haaland lilimfanya kufikisha mabao 10 kwenye Ligi Kuu aliyoifungia Dortmund kwenye mechi saba msimu huu.

# Xavi: Barca haikustahili ushindi kwa Villarreal



**BARCELONA, Hispania**

XAVI anaamini ushindi wa Barcelona wa mabao 3-1 dhidi ya Villarreal utawapa morali zaidi wachezaji wake licha ya kutambua ukweli kwamba, kiwango cha timu hiyo hakikuwa cha kuvutia kuweza kupata pointi tatu.

Kiungo huyo wa zamani wa Barca, alianza kuinoa timu hiyo kwenye ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Espanyol wikiendi iliyopita baada ya kuchukua mikoba ya Ronald Koeman, lakini ilionekana kama wasingepata ushindi juzi Jumamosi wakati Samuel Chukwueze aliposawazisha bao la uongozi la Frenkie de Jong.

Memphis Depay alifunga bao la pili dakika ya 88, kabla ya Philippe Coutinho kuongeza la tatu kwa mkwaju wa penalti.

Si tu ulikuwa ushindi wa kwanza wa Barca kushinda ugenini kwenye mchezo wa LaLiga msimu huu, pia ilikuwa ni mara ya kwanza wakishinda mara mbili mfululizo kwenye ligi hiyo msimu huu.

Ushindi dhidi ya Espanyol ulifuatiwa na suluhu dhidi ya Benfica kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati ya wiki, na Xavi amesema ushindi huo pale La Ceramica ulikuwa muhimu baada ya timu yake kucheza vibaya kwenye mechi tatu katika mashindano yote tangu aanze kuinoa.

"Ilikuwa si rahisi, Villarreal ni timu kubwa," Xavi alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kiukweli katika michezo yote tuliyocheza ni mmoja tu ndio tulitawala kwa asilimia kubwa na huo ndio haswa tulistahili kushinda.

"Leo (juzi) tungeweza kumaliza kwa sare na badala yake tumetoka na ushindi. Kwa uhakika imetupa sisi morali kubwa zaidi."

LIVE IN PLAY

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA

PAKUA SASA

# UTOTO WAMKERA KOCHA MBEYA CITY



**Na Dennis Fussi**

KOCHA wa Mbeya City, Mathias Lule, amesema utoto uliiponza timu yake na kujikuta ikilazimishwa sare ya kufungana mabao 2-2 na KMC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Jumamosi.

Katika mchezo huo, uliopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokione jijini Mbeya, KMC walitoka nyuma mara mbili na kusawazisha mabao hayo na kulazimisha kugawana pointi moja-moja.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Lule alisema wachezaji wake walifanya 'utoto' kwenye mchezo huo na ndio sababu wakashindwa kuondoka na ushindi wa pointi zote tatu.

Hata hivyo, Lule ambaye ni raia wa Uganda, alisema hawezi kumlaumu mchezaji mmoja mmoja, lakini ukweli ni kwamba walifanya utoto na kushindwa kupata matokeo waliyoyahitaji.

"Siwezi kutaja mchezaji mmoja mmoja kuwa ndio alifanya utoto kwenye mchezo wa leo (juzi), lakini ni jambo la wazi kabisa tulicheza vibaya na tumeshindwa kupata pointi tatu," alisema Lule.

Aidha, alisema kwamba, baada ya mtokeo hayo sasa wanakwenda kukaa na kusawazisha makosa yao ili utoto huo usijitokeze tena kwenye mechi zinazofuata.

"Haya tunayaacha hapa, sasa tunakwenda kuangalia namna ya kumaliza utoto na uzembe ili tusirudie makosa kwenye mchezo ujao," alisema.

Baada ya matokeo hayo Mbeya City sasa ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi ikiwa na pointi 11, huku KMC ikiwa naafasi ya 14 na alama zake sita wakati huu zote zikishuka dimbani mara saba.



# Baraza ataja kilichoiua Kagera Sugar ugenini

**Na Dennis Fussi**

KOCHA wa Kagera Sugar, Francis Baraza, amesema sababu ya timu yake kupoteza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting ni uzembe wa wachezaji wake.

Mchezo huo ulipigwa Novemba 26 na Kagera ikachezea kichapo cha mabao 2-1 licha ya kutangulia kuwa mbele.

Kwa mujibu wa Baraza, ambaye ni raia wa Kenya, walitarajia kushinda mchezo huo, lakini wenyeji wao Ruvu walipambana hadi dakika ya mwisho na kupata pointi zote tatu.

Alisema walicheza vizuri, lakini uzembe ndio ulichangia kwa wao kupoteza, kwani walikuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata ushindi.

"Tuliuanza mchezo vizuri na kupata bao la mapema, lakini wachezaji wangu waliridhika na tukawapa nafasi wenyeji wetu kutushambulia na kufunga mabao mawili," alisema Baraza.

Huo ni mchezo wa pili mfululizo kwa Kagera Sugar kupoteza baada ya kutoka kufungwa nyumbani mabao 2-1 na Geita Gold.

Kabla ya mechi za jana, Kagera wapo nafasi ya saba kwenye msimamo wakiwa na pointi nane, huku Ruvu wakiwa nafasi ya sita na alama tisa 9 baada ya kushuka dimbani mara saba.

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 29 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3572 | Estoril Praia U23 vs Sporting CP U23 | 1.77 | 3.71 | 3.76 |
| 15:00 | 3110 | Mladost DG vs Berane | 1.96 | 2.98 | 3.94 |
| 15:00 | 4355 | Gabala vs Karabakh | 6.18 | 3.77 | 1.49 |
| 16:00 | 3094 | Charlton U23 vs QPR U23 | 2.22 | 4.14 | 2.46 |
| 16:00 | 5800 | Hamburger II vs Holstein Kiel II | 2.44 | 3.55 | 2.44 |
| 16:30 | 5489 | Albinoleffe vs Piacenza Calcio | 1.73 | 3.43 | 4.97 |
| 16:45 | 4779 | Pusamania Borneo vs Persija Jakarta | 2.69 | 3.27 | 2.37 |
| 17:00 | 1666 | ASM Oran vs MCB Oued Sly | 2.06 | 2.88 | 3.75 |
| 17:00 | 2432 | GC Mascara vs MC Saida | 1.78 | 3.18 | 4.44 |
| 17:00 | 4354 | US Chaouia vs CA Batna | 1.67 | 3.33 | 5.01 |
| 17:00 | 4647 | Northeast United FC vs Chennaiyin FC | 2.14 | 3.23 | 3.09 |
| 17:00 | 4683 | Novi Pazar vs Proleter | 2.46 | 3.38 | 2.51 |
| 17:00 | 5077 | WA Boufarik vs RC Kouba | 2.20 | 2.84 | 3.42 |
| 17:00 | 5252 | JSM Bejaia vs USM Khenchela | 3.23 | 2.80 | 2.31 |
| 17:00 | 5376 | USM EL Harrach vs JSM Tiaret | 1.70 | 3.27 | 4.81 |
| 17:00 | 5640 | Ufa vs Spartak Moscow | 3.47 | 3.33 | 2.03 |
| 18:15 | 4653 | Ludogorets Razgrad vs CSKA Sofia | 1.97 | 3.38 | 3.38 |
| 18:30 | 3072 | Gaz Metan Medias vs Farul Constanta | 3.70 | 3.20 | 2.01 |
| 18:45 | 3517 | Anorthosis Famagusta vs Apollon Limassol | 2.72 | 3.37 | 2.47 |
| 19:00 | 4280 | Vojvodina vs Mladost Lucani | 1.57 | 3.77 | 5.02 |
| 19:00 | 4968 | Arsenal Tula vs Lokomotiv Moscow | 3.25 | 3.44 | 2.08 |
| 20:00 | 2897 | Goeztepe vs Fenerbahce | 3.45 | 3.45 | 2.02 |
| 20:00 | 5093 | Tuzlaspor vs Erzurum BB | 3.12 | 3.36 | 2.07 |
| 20:00 | 5968 | Slovan Bratislava vs SKF Sered | 1.13 | 7.14 | 13.51 |
| 20:30 | 2714 | Oleksandria vs Zorya Lugansk | 2.85 | 3.28 | 2.25 |
| 21:00 | 1476 | Apoel Nicosia vs Omonia Nicosia | 2.32 | 3.32 | 2.97 |
| 21:00 | 2099 | CF Estrela vs Benfica Lisbon B | 2.30 | 3.51 | 2.73 |
| 21:00 | 2992 | Turkgucu Ataspor Munchen vs Zwickau | 2.37 | 3.25 | 2.86 |
| 21:00 | 3339 | Elfsborg vs AIK Football | 2.17 | 3.23 | 3.04 |
| 21:00 | 5519 | Sirius FK vs BK Hacken | 2.94 | 3.47 | 2.12 |
| 21:00 | 5668 | Mjallby vs Orebro SK | 1.36 | 4.63 | 6.75 |
| 21:00 | 5688 | Vejle BK vs Midtjylland | 6.11 | 4.53 | 1.45 |
| 21:30 | 3583 | CFR Cluj vs Clinceni | 1.12 | 7.08 | 21.62 |
| 22:00 | 2290 | Sunderland U23 vs Nottingham U23 | 4.55 | 4.06 | 1.58 |
| 22:00 | 3543 | Manchester City U23 vs Leeds United U23 | 1.67 | 4.05 | 3.95 |
| 22:00 | 4292 | Kecskemeti TE vs Haladas | 2.55 | 3.03 | 2.65 |
| 22:00 | 5281 | Wolverhampton U23 vs Norwich U23 | 1.99 | 3.72 | 3.04 |
| 22:00 | 5336 | Reading U23 vs Middlesbrough U23 | 3.50 | 3.79 | 1.81 |
| 22:00 | 5623 | Birmingham U23 vs Fulham U23 | 6.73 | 5.19 | 1.32 |
| 22:00 | 5650 | Emmen vs Almere City | 1.56 | 4.28 | 4.77 |
| 22:30 | 5492 | Ternana vs Crotone | 1.84 | 3.58 | 3.87 |
| 22:30 | 5772 | Cerro Largo FC vs Torque | 2.69 | 3.51 | 2.26 |
| 22:45 | 2959 | Brechin City vs Darvel FC | 2.42 | 3.67 | 2.42 |
| 22:45 | 3341 | Derby vs QPR | 2.75 | 3.24 | 2.45 |
| 23:00 | 2023 | Eibar vs Girona | 2.03 | 3.24 | 3.58 |
| 23:00 | 2029 | Osasuna vs Elche | 1.83 | 3.36 | 4.61 |
| 23:00 | 3924 | Juve Stabia vs Taranto Sport | 2.17 | 3.21 | 3.36 |
| 23:00 | 4557 | Union Santa Fe vs Atletico Tucuman | 1.78 | 3.37 | 4.14 |
| 23:00 | 5494 | Sportivo Barracas vs Puerto Nuevo | 2.30 | 3.35 | 3.05 |
| 23:15 | 4086 | GD Estoril vs Santa Clara | 2.01 | 3.22 | 3.76 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Novemba 29, 2021

Nipashe




Arteta aanika siri ya ushindi Arsenal

UKURASA 21

KIJIJI...



Winga wa Simba, Bernard Morrison 'Wakili Msomi', akikichambua 'kijiji' cha safu ya ulinzi ya Red Arrows ya Zambia kabla ya kutoa pasi ya mwisho kwa Meddie Kagere, aliyeiandikia timu yake bao la pili wakati wakishinda 3-0 kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Refa mechi Yanga, Namungo 'kizimbani'

**Na Adam Fungamwango**

MWAMUZI Abel William kutoka Arusha, aliyechezesha mechi ya Ligi Kuu namba 45 kati ya Namungo na Yanga kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi, Novemba 20, mwaka huu, wakati timu hizo zitoka sare ya bao 1-1, amepelekwa kwenye Kamati ya Waamuzi kwa ajili ya kujadiliwa.

Taarifa iliyotolewa jana na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) katika kikao chake kilichokaa Novemba 26, mwaka huu na kupitia mwenendo na matukio mbalimbali ya ligi, imefanya uamuzi wa kumpeleka mwamuzi huo kwa kile kilichotajwa kuwa ilijiridhisha kuwa mchezo husika ulikumbwa na matukio ya maamuzi walioacha maswali juu ya utekelezaji wa sheria namba 17 za mpira wa miguu.

"Mwamuzi wa kati wa mchezo wa Namungo dhidi ya Yanga, Abel William kutoka Arusha amepelekwa Kamati ya Waamuzi ili shauri lake likajadiliwe na kamati hiyo.

Uamuzi huo umekuja baada ya kamati hiyo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi Kuu kujiridhisha kuwa mchezo husika ulikumbwa na matukio na maamuzi yalioacha maswali juu ya utekelezaji wa sheria 17 za mpira wa miguu," ilieleza taarifa hiyo.

Kamati hiyo imetoa onyo kali kwa wachezaji wa Namungo FC, Jacob Massawe na Lucas Kikoti na Bigirimana Blaise ambao kwa nyakati tofauti walionyesha utovu wa nidhamu kwa vitendo na lugha zisizo na staha.

# MORRISON SHUJAA SIMBA IKITANGULIZA MGUU CAF

●●●Aiongoza kuirarua Red Arrows mabao matatu kwa Mkapa, sasa wahitaji sare kutinga makundi huku...

**Na Adam Fungamwango**

AKIWA kwenye kiwango bora zaidi pengine kuliko alichowahi kukionyesha tangu ajiunge na klabu ya Simba mwaka 2020, winga Bernard Morrison aliiwezesha timu hiyo kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, alipofunga mabao mawili na kutoa pasi moja, wakati ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Red Arrows, Uwanja wa Benjamin Mkapa jana.

Pamoja na kukosa mkwaju wa penalti, Morrison alikuwa kivutio uwanjani hapo na mashabiki na waliokuwa wakiangalia soka kwenye televisheni, huku akiwa mchezaji aliyekuwa na uwezo wa kuipenya anavyotaka ngome ya Red Arrows.

Ni mechi iliyokumbushia mwaka 2018, mara ya mwisho Simba ikicheza Kombe la Shirikisho kwenye uwanja huo Machi 7, 2018, ikicheza dhidi ya Al Masry ya Misri na kutoka sare ya mabao 2-2, huku mvua kubwa ikinyesha na kusababisha mechi hiyo kuahirishwa kwa muda, ndivyo ilivyokuwa pia jana, ikicheza kwa mara ya kwanza kombe hilo baada ya miaka mitatu kupita.

Mechi ilianza huku mvua kubwa iliyoanza kunyesha Dar es Salaam tangu juzi, maji yakionekana kutuama baadhi ya maeneo ya uwanja huo hasa upande wa magharibi mwa uwanja na kuwapa wakati mgumu wachezaji wa pande zote mbili.

Wachezaji walionekana kuteleza wanapokimbilia mpira, na mpira kutofika sehemu ambayo pasi imekusudiwa.

Ilichukua dakika 14 timu kufanya shambulizi, wakati Hassan Dilunga alipoingia ndani ya eneo la hatari na kupiga shuti lililodakwa na kipa Charles Kalumba.

Dakika mbili baadaye Simba iliandika bao la kwanza lililofungwa na Morrison kwa mkwaju wa faulo, uliotokana na yeye mwenyewe kuvutwa jezi nje kidogo ya eneo la hatari.

Morrison alipiga faulo iliyogonga nguzo ya pembeni kushoto mwa kipa Kalumba na kujaa wavuni upande wa kulia.

Kuingia kwa bao hilo kulionekana kuwaduwaza Red Arrows na kuwafanya wapinzani wao wapeleke mashambulizi kama nyuki.

Dakika tatu baadaye, Morrison tena, aliwafungasha tena mabeki wa Wazambia hao na kuwachambua kama karanga, nje hadi ndani ya eneo la hatari, kabla ya kutoa krosi fupi iliyomkuta Meddie Kagere akiwa peke yake na nyavu, akausukumiza mpira wavuni.

Simba ilipata penalti dakika ya 33, baada ya Dilunga kusukumwa ndani ya eneo la hatari, lakini Morrison alipiga penalti dhaifu iliyopanguliwa na kipa Kalumba.

Red Arrows walifanya shambulizi la kwanza la hatari langoni mwa Simba dakika tano kabla ya mapumziko, baada ya faulo iliyopigwa na Alassane Diarra iliyotua kichwani mwa Benedict Chepeshi, lakini kichwa chake kilipaa juu kidogo ya lango.

Straika hatari wa timu hiyo, James Chamanga aliunganisha krosi iliyopigwa upande wa kushoto, lakini mpira ulitoka nje kidogo langoni mwa Simba.

Kipindi cha pindi cha pili, Simba iliwatoa Dilunga, Sadio Kanoute, na kuwaingiza Mzamiru Yassin na Ibrahim Ajibu, huku Peter Banda akiingia mwishoni kabisa mwa mchezo.

Morrison alifunga bao la tatu dakika ya 77, alipoupata mpira wa kurushwa, akitoka pembeni mwa uwanja na kuingia nao ndani, kabla ya kumpiga tobo kipa Kalumba, ukajaa wavuni.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >